NURU YA MAHUJAJI

KWA NURU YA QUR-AN NA SUNNA NA MSAADA KWA TAASISI ZA MAHUJAJI

MTUNZI

ABUU MUHAMMAD

HASNUU AMOUR KOMBO

AZZINJIBARY ATTANZANIY



مكتبة
الإمام الأوزاعي بالزنجباري

NURU YA MAHUJAJI KWA NURU YA QUR-ANI NA SUNNA
NA
MSAADA KWA TAASISI ZA MAHUJAJI

MTUNZI

ABUU MUHAMMAD HASNUU AMOUR KOMBO

AZZINJIBARY ATTANZANIY

Kitabu hichi ni haki ya mmiliki (muandishi) na si ruhusa kutowa kopi isipokua kwa ruhusa ya mwenye kitabu.

(m) Abuu Muhammad Hasnuu Amour

Kimeandikwa kitabu hichi tarehe 27/12/2018 na kuchapishwa na kutolewa tarehe 6/6/2020 na kimechapishwa Maktabatul Imamil Auzaai'y Zanzibar.

KITABU CHA HIJJA/ ABUU MUHAMMAD HASNUU

+255779-819880

0772 719464 - 0776 959197

ZANZIBAR-TANZANIA

YALIYOMO

1. UTANGULIZI.....UK (4)
2. SABABU YA KUANDIKA KITABU HICHI.....UK (6)
3. UWAJIBU WA IBADA YA HIJJA.....UK (7)
4. ADABU NA TABIA NJEMA KWA MWENYE KUFANYA HIJJA.....UK(8)
5. SHARTI ZA KUMUWAJIBIKIA MTU IBADA YA HIJJA.....UK(15)
6. NASAHA MUHIMU KWA KILA TAASISI ZA MAHUJAJI.....UK(21)
7. NASAHA KWA KILA MWANAMKE ALIYEKUSUDIA KUFANYA IBADA YA HIJJA .....UK(23)
8. AINA ZA IBADA YA HIJJA.....UK(23)
9. VITUO VYA KUHIRIMIA.....UK(25)
10. MATENDO YA MWENYE KUTAKA KUFANYA UMRA.....UK(28)
11. NASAHA KWA MAHUJAJI.....UK(29)
12. NASAHA KWA WANAWAKE MAHUJAJI.....UK(35)
13. MAMBO AMBAYO SI MAKOSA KWA MUHRIM.....UK(36)
14. MAMBO AMBAYO YAMEHARAMISHWA KWA MUHRIM.....UK(39)
15. NAMNA YA KUFANYA U'MRA.....UK(46)
16. TWAWAFU YA U'MRA.....UK(46)
17. BAADHI YA MAKOSA YANAYOFANYWA KATIKA TWAWAFU.....UK(50)
18. BAADA YA KUMALIZA TWAWAFU.....UK(52)
19. BAADHI YA MAKOSA YANAYOFANYWA KATIKA SA'AYI.....UK(55)
20. BAADA YA HUJAJI KUMALIZA SA'AYI.....UK(56)
21. NAMNA YA KUTEKELEZA HIJJA.....UK(58)
22. KUELEKEA A'RAFA.....UK(59)
23. KUSIMAMA A'RAFA.....UK(62)
24. BAADHI YA MAKOSA YANAYOFANYWA KATIKA A'RAFA.....UK(65)
25. KULALA MUZDALIFA.....UK(66)
26. MATENDO YA SIKU YA IDDI.....UK(68)
27. KUTUPA VIJIWE JAMARATUL A'QABA.....UK(69)
28. KUCHINJA SIKU YA IDDI.....UK(72)
29. KUPUNGUZA NYWELE AU KUNYOA.....UK(74)
30. TWAWAFUL IFADHA.....UK(78)
31. NAMNA YA KUTEKELEZA TWAWAFUL IFADHA.....UK(79)
32. KULALA MINA.....UK(80)
33. UFAFANUZI NA UBAINIFU WA KULALA MINA.....UK(81)
34. KUTUPA VIJIWE KATIKA VIKUTA AU NGUZO.....UK(83)
35. KUFANYA HARAKA KUONDOKA MWEZI 12.....UK(85)
36. TWAWAFUL WADAA.....UK(86)
37. ZIARA YA MISIKITI MITUKUFU.....UK(89)
38. SWALA YA MAITI NDANI YA MISIKITI MITUKUFU.....UK(95)
39. NAMNA YA KUSWALI SWALA YA MAITI.....UK(96)
40. MANENO YA MWISHO YA MTUNZI.....UK(99)

بسم الله الرحمن الرحيم

UTANGULIZI

Kila sifa njema na shukrani zote anastahiki kusifiwa na kushukuriwa Allah (Subahaanahu wata'ala) ambaye ni Muumba wa kila kitu, na ni mwenye kustahiki kuabudiwa na kila kitu na kutoshirikishwa na kitu chochote.

Swala na salamu nyingi na kwa ukamilifu wake ziwe kwa Mtume wetu kipenzi Muhammad na ali zake na wale wote waliyowafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

Ama baada ya shukrani hizo na kumtakia swala na salamu Bwana Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam), hichi ni kitabu ambacho kinachoelezea na kuelimisha juu ya Ibada ya Hijja kwa mujibu wa Qur-ani na Sunna za Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) kwa ufahamu wa wema waliotangulia.

Na kitabu hichi tumekipa jina **"NURU YA MAHUJAJI KWA NURU YA QUR-ANI NA SUNNA NA MSAADA KWA TAASISI ZA MAHUJAJI"**

Tukiwa tunakusudia katika jina hilo ya kwamba hichi kitabu ni nuru kwa Mahujaji endapo watakua ni wenye kukisoma kitawaangazia na kuwaelimisha mas-ala mazima ya Ibada ya Hijja kwa kupitia elimu yenye nuru katika Qur-ani na Sunna za Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) kwa ufahamu wa wema waliotangulia, na ni msaada kwa zile taasisi ambazo

zinazosimamia Mahujaji katika kuhakikisha Ibada za mahujaji hao zinatekelezwa vizuri, kwa hiyo kitabu hichi kitawasaidia hao wasimamizi wa taasisi hizo katika kazi yao hii ya kuwashuhulikia waisilaamu katika kutimiza na kutekeleza Ibada yao hii iliyo kubwa.

Tunamuomba Allah kwa majina yake matukufu aifanye kazi hii iwe na Ikh-lasi na iwe na Baraka nyingi kutoka kwake na awanufaishe waisilamu wote kupitia kitabu hichi.

Aamin.

ABUU MUHAMMAD HASNUU AMOUR KOMBO

AZZINJIBARY ATTANZANIY

SABABU YA KUANDIKA KITABU HICHI

Baada ya utangulizi huo, ni vyema kuelezea japo kwa ufupi kuhusu sababu iliyonipelekea kuandika kitabu hichi nazo ni sababu mbili hizi zifuatazo:

a) **Sababu ya kwanza:** Ni kuwa nimejaribu kuangalia na kuvipitia vitabu vingi vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili ambavyo vimeandikwa kwa kuelezea Ibada hii ya Hijja, baadhi yake vimeelezea kwa ufupi mno na vyengine vimeelezea mambo yaliyokuwa hayamo katika usahihi. Kwa hiyo nimeonelea ni vyema kukiandika kitabu hichi ili iwe ni muangaza kwa wale wanaotarajia kuitekeleza Ibada ya Hijja ili watekeleze katika usahihi wake.

b) **Sababu ya pili:** Ni kuwa Allah (Subahaanahu wata'ala) ameniruzuku katika mwaka wa kiisilamu 1439 mwishoni mwa huo mwaka ambao sawa na mwaka wa kizungu 2018, ameniruzuku kwenda kutekeleza Ibada ya Hijja na baada ya kufika katika miji mitakatifu ya Makka na Madina, kuna vitu vingi baadhi yetu walikuwa wakivifanya na ilhali ni makosa na vyengine ambavyo vilivyohimizwa baadhi yetu walizembea kuvitekeleza ipasavyo. Kwa hiyo na hii pia ikawa ni miongoni mwa sababu ya kuandika kitabu hichi ili iwe ni muangaza wa kuondoa ujinga uliowavaa watu katika Ibada hii ya Hijja.

Namuomba Allah (Subahaanahu wata'ala) akitie Qabuli kitabu hichi kiwe ni taa katika Ibada hii ya Hijja kwa wanaotarajia kutekeleza Ibada hii.

Aamin.

UWAJIBU WA IBADA YA HIJJA

Ibada ya Hijja ni wajibu kwa kila Muisilamu aliye baleghe, mwenye akili timamu na aliyeruzukiwa uwezo wa mali ambayo itamfikisha katika miji mitakatifu kwa ajili ya kuitekeleza Ibada hiyo pamoja na kufungamana na mali hiyo na sharti ya kua iwe ni halali mali hiyo, na dalili ya hayo ni hizi zifuatazo:-

1. Katika Qur-ani amesema Allah (Subahaanahu wata'ala):

﴿ فِيهِ ءَايَٰتُۢ بَيِّنَٰتٌ مَّقَامُ إِبۡرَٰهِيمَۖ وَمَن دَخَلَهُۥ كَانَ ءَامِنٗاۗ وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلۡبَيۡتِ مَنِ ٱسۡتَطَاعَ إِلَيۡهِ سَبِيلٗاۚ وَمَن كَفَرَ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنِ ٱلۡعَٰلَمِينَ ﴾

[آل عِمۡرَان : ٩٧] .

"Na kwa ajili ya Allah imewaajibikia watu wahiji kwenye nyumba hiyo (iliyopo Makka) kwa yule awezae njia ya kuendea na atakaekanusha basi Allah si muhitaji kwa walimwengu".
(Al-imran: 97)

Amesema Ibnu Kathir katika kuitolea maana aya hii katika kitabu chake cha tafsiri kwa kusema:

{تَدُلُّ الآيَةُ عَلَى وُجُوْبِ الحَجِّ عِنْدَ الجُمْهُوْرِ}.

"Hii aya (inajuulisha kua) ni wajibu kuhiji mbele ya wengi katika wanazuoni"

Nimesema hapa: Hijja ni wajibu wala hakuna khilafu.

2. Dalili katika hadithi ni kauli yake Mtume (Swallallahu ‘alayhi wasallam) pale aliposema:

﴿... وَتَحُجَّ البَيْتَ إِنِ اسْتَطَعْتَ إِلَيْهِ سَبِيْلاً ﴾.

“Na kwenda kuhiji nyumba ya Alqaaba ikiwa utakuwa na uwezo wa kuielekea njia ya kufika huko” (Muslim: 93)

Kwa hiyo, Ibada ya Hijja ni nguzo ya tano katika nguzo za Kiisilamu na ni wajibu kuitekeleza katika umri wa Muisilamu mara moja tu na mara zitakazo bakia ikiwa Muisilamu atatekeleza zaidi ya mara moja ni Sunna. Na ni wajibu kwa Muisilamu akimbilie kuitekeleza Ibada hii pindi tu anapopata uwezo kwa kuchelea mauti yasijempata kabla hajaitekeleza.

ADABU NA TABIA NJEMA AMBAZO ANATAKIKANA AWE NAZO MWENYE KUFANYA IBADA YA HIJJA NA UMRA

Miongoni mwa adabu na tabia njema ambazo anatakikana awe nazo yoyote yule aliyekusudia kuifanya Ibada ya Hijja ni hizi zifuatazo:-

1) Kuyasafisha kabisa matendo yake na kuyatakasa kwa ajili ya Allah na kusalimika kutokana na riyaa na kutaka kusikilikana ili iwe ni sababu kwa kufanya hivyo kutimiza lengo la hijja nalo ni kurudi nyumbani hali ya kua amefutiwa dhambi zake zote kama kwamba ndo kwanza amezaliwa na mama yake, akiwa hali hiyo

basi huyo anakua amekubaliwa matendo yake yote na kinyume chake ni kukataliwa matendo yake.

وَعَنْ أَبِيْ هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُوْلُ اللهِ ﷺ: قَالَ اللهُ تَبَارَكَ وَتَعَالَى: « أَنَا أَغْنَى الشُّرَكَاءِ عَنِ الشِّرْكِ مَنْ عَمِلَ عَمَلاً أَشْرَكَ فِيْهِ مَعِيْ غَيْرِي تَرَكْتُهُ وَشِرْكَهُ » (رواه مسلم: ٢٩٨٥)، (وابن ماجة: ٤٢٠٢).

“ Kutoka kwa Abuu Hurayra (radhiyallahu a’nhu) amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam) Amesema Allah (Subahaanahu wata’ala): “Mimi ni mkwasi nimetosheka sihitaji washirika kutokana na kushirikishwa, basi yeyote atakaefanya matendo akanishirikisha ndani ya matendo hayo pamoja na mimi mwengine, nitamuachia (matendo yake hayo akalipwe) na mshirika wake ”.

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu): Hadithi hii inahimiza kujipamba na Ikh-las nayo ni kusafisha matendo na kuyatakasa iwe kwa ajili ya Allah tu iwe ni sababu ya kuyakubali matendo hayo.

2) Kujitahidi mwenye kukusudia kufanya Ibada ya Hijja na Umra katika kujielimisha na kutambua hukumu za Hijja na Umra ili aitekeleze Ibada yake hii kwa elimu.
Na dalili ya hili ni kauli yake Allah (Subahaanahu wata’ala) pale aliposema:

﴿ صِرَٰطَ ٱلَّذِينَ أَنۡعَمۡتَ عَلَيۡهِمۡ غَيۡرِ ٱلۡمَغۡضُوبِ عَلَيۡهِمۡ وَلَا ٱلضَّآلِّينَ ﴾

[الفَاتِحَة : ٧]

“Njia ya wale ambao umewaneemesha juu yao sio ya waliokasirikiwa juu yao na wala waliopotea”.
Hapa wanakusudiwa Mayahudi na Manaswara na mfano wa hao na ndo maana wamesema Ahlul-ilmi (wanachuoni) juu ya aya hii:

{ اليَهُوْدُ فَقَدُوا العَمَلَ وَالنَّصَارَى فَقَدَ العِلْمَ وَلِهَذَا كَانَ الغَضَبُ لِلْيَهُودِ وَالضَّلاَلُ لِلنَّصَارَى } .

“Na mayahudi walikosa kufanyia kazi elimu waliyopewa ndio ikawa sababu ya kukasirikiwa na wanaswara wamekosa elimu wakawa wanafanya matendo bila ya elimu ndo ikawa sababu ya kupotea”
Kwa hiyo kua na elimu na jambo unalolifanya ni muhimu na ni lazima na mwenye kufanya Ibada ya Hijja ni lazima kujipamba na tabia hii na sifa hii.

3) Kujihimiza katika safari yake ya kuelekea miji mitakatifu ya Makka na Madina kusuhubiana [(1)] na watu wa kheri ambao atapata faida kutoka kwao faida za kielimu na za kiadabu nzuri.

---

1. Maana ya kusuhubiana ni kushikamana nao na kufuatana nao.

وَعَنْ أَبِي مُوْسَى الأَشْعَرِيّ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: « مَثَلُ الجَلِيْسِ الصَّالِحِ وَالسُّوْءِ كَحَامِلِ المِسْكِ وَنَافِخِ الكِيْرِ، فَحَامِلُ المِسْكِ إِمَّا أَنْ يَهْدِيَكَ أَوْ أَنْ تَبْتَاعَ مِنْهُ وَإِمَّا أَنْ تَجِدَ مِنْهُ رِيْحًا طَيِّبَةً، وَنَافِخُ الكِيْرِ إِمَّا أَنْ يُحْرِقَ ثِيَابَكَ وَإِمَّا أَنْ تَجِدَ رِيْحًا خَبِيْثَةً » (رواه البخاري: ٥٥٣٤) و (مسلم: ٢٦٢٨).

“Kutoka kwa Abuu Muusa Al-ash-ariyy (radhiyallahu a’nhu) kutoka kwa Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam) Amesema: “Mfano wa rafiki mwema na rafiki m-baya ni mfano wa muuza mafuta ya miski na mfua vyuma, basi muuza mafuta mazuri ukiwa umesuhubiana nae imma atakupa zawadi hayo mafuta (hiba) na imma utanunua kutoka kwake mafuta na imma utapata harufu nzuri kupitia hayo mafuta anayouza, na mfua vyuma imma ataunguza nguo zako na imma utapata harufu mbaya kupitia kazi yake ya kufua vyuma”.

Hii hadithi inahimiza watu washikamane na marafiki wazuri na wema na kuwa mbali na marafiki wabaya na waovu katika hali zao zote za maisha yao, kwa hiyo kwa mwenye kufanya ibada ya Hijja ni vyema kujipamba na jambo hili mapema.

4) Achukue pamoja na yeye katika safari yake ya kwenda kuhiji pesa zitakazomtosheleza kwa mahitaji yake ili asije akahitaji mali zilizomo mikononi mwa watu.

Hii vile vile ni tabia njema ambayo Hajji anatakiwa ajipambe nayo asitamani vilivyomo mikononi mwa watu bali akinai na alichoruzukiwa na Allah (Subahaanahu wata'ala).

وَعَن أَبِي سَعِيْدِ الخُدْرِيّ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ ﷺ قَالَ: « وَمَنْ يَسْتَعِفَّ يُعِفُّهُ اللهُ وَمَنْ يَسْتَغْنِ يُغْنِهِ اللهُ » (رواه البخارى: ١٤٦٩) و (مسلم: ١٠٥٣).

"Kutoka kwa Abuu Saiid Al-khudriy (radhiyallahu a'nhu), kutoka kwa Mtume wa Allah (Swallallahu a'layhi wasallam) amesema: "Na yeyote atakaejizuilia na kuomba, Allah atamlipa juu ya kujizuilia kwake huku kwa kumpa badili na kheri, na yeyote atakaejitosheleza na Allah akawa anamuhitajia Allah na wala akawa hamuhitaji mwengine basi Allah atamtoshelezesha"

Basi ewe mwenye kukusudia ibada ya Hijja jiepushe na sifa mbaya ya kuomba wakati unapokuwepo katika miji mitakatifu na ili uepukane na tabia hii mbaya ni vyema kuchukuwa pesa zitakazokutoshelezesha kwa mahitaji yako.

5) Kujipamba na tabia nzuri na kuamiliana na wengine muamala uliokuwa mzuri kwani katika ibada ya Hijja unakutana na watu wengi na unachanganyika na wengi na kila mmoja huwa na tabia zake alizotoka nazo nyumbani kwa hiyo changanyika nao kwa tabia nzuri.

وَعَنْ أَبِي ذَرٍّ الغِفَارِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُوْلُ اللهِ ﷺ: « اتَّقِ اللهَ حَيْثُ مَا كُنْتَ، وَأَتْبِعِ السَّيِّئَةَ الحَسَنَةَ تَمْحُهَا، وَخَالِقِ النَّاسَ بِخُلُقٍ حَسَنٍ » (رواه الترمذي: ١٩٨٧) ، (وأحمد: ٢١٣٩٢) وَحَسَّنَهُ الأَلْبَانِيُّ فِي صَحِيْحِ سُنَنِ التِّرْمِذِيِّ وَصَحِيْحِ التَّرْغِيْبِ.

Na kutoka kwa Abuu Dharri Al-ghifaariy (radhiyallahu a’nhu) amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam): “Muogope Allah popote pale ulipo na fuatilishia ovu kwa jema, litafuta hilo ovu na changanyika na watu kwa tabia njema (nzuri)”.

Katika hadithi hii Mtume anahimiza kuamiliana na watu kwa tabia nzuri na njema kwani ndani yake kuna mafanikio makubwa, kwa hiyo ewe mwenye kukusudia kufanya ibada ya Hijja lifahamu hili uwe pahala pazuri zaidi.

6) Kutahadhari na kuwaudhi wengine utakapokua katika ibada ya Hijja imma kwa kuwatukana au kuwatolea maneno makali yatakayopelekea kuingia kitu ndani ya nafsi imma kuwapiga au kuwachukulia vitu vyao kwa dhulma.

Tahadhari na mambo hayo kwani haya yanaharibu ibada na si katika tabia za muisilamu wa kweli.

وَعَنْ عَبْدِ اللهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ ﷺ قَالَ: « الْمُسْلِمُ مَنْ سَلِمَ الْمُسْلِمُوْنَ مِنْ لِسَانِهِ وَيَدِهِ » (رواه البخاري: ١٤٦٩) و (مسلم: ١٠٥٣).

“Kutoka kwa Abdillahi bin Amru (radhiyallahu a’nhu), kutoka kwa Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam) amesema: “Muisilamu ni yule ambae wamesalimika waisilamu wenzake kutokana na ulimi wake na mkono wake”.

Wanasema wanachuoni “Muisilamu wa uhakika ni yule ambae panadhihirika kwake athari za Uisilamu na matukufu yake huo Uisilamu na hua anazuia maudhi ya ulimi wake na maudhi ya mikono yake kutowafika waisilamu wenzake, kwa hiyo huwa hapadhihiri kwake isipokua maneno mazuri na vitendo vizuri kwa ndugu zake waisilamu”.
Kwa mwenye kufanya ibada ya Hijja jambo hili ajitahidi sana kwani hukutana na kila aina ya maudhi kwa hiyo yeye asirejeshe maudhi bali awe ni mpole na kua mstahamilivu sana pamoja na kuvumilia.

7) Kujishughulisha sana na jambo la kumtaja Allah, kumuomba dua kwa wingi na kuomba msamaha pamoja na kuhifadhi ulimi wake isipokua katika maneno ya kheri na kutumia wakati wake katika mambo ambayo mwisho wa mambo hayo atakuwa ni mzuri duniani na akhera.

وَعَنْ أَبِيْ هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُوْلُ اللهِ ﷺ: « مَنْ كَانَ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الآخِرِ فَلْيَقُلْ خَيْرًا أَوْ لِيَصْمُتْ ».

Na kutoka kwa Abuu Hurayra (radhiyallahu a'nhu) amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallallahu a'layhi wasallam): "Yeyote mwenye kumuamini Allah na siku ya mwisho basi aseme maneno ya kheri au anyamaze".

Mafunzo ya hadithi hii ni kua ikiwa unataka kuzungumza basi zungumza yaliyo ya kheri na kama huna la kuzungumza basi ni vyema kunyamaza kimya, kwani kunyamaza kimya kuna kheri nyingi, na ukihisi umeleta adhkari na mwili umechoka basi vilevile ni vyema ukapumzike kuliko kufungua baraza ya mazungumzo kwani baraza hiyo huenda ikawa pahala pabaya pa kuharibu ibada yako, zinduka juu ya hili ewe mwenye kuitaka kheri na kuikimbia shari.

Hizi ni adabu na tabia ambazo anatakikana Muisilamu afanye pupa kujipamba nazo katika hali zake zote na haswa haswa katika safari ya kuelekea kwenda kufanya ibada ya Hijja na Umra.

SHARTI ZA KUMUWAJIBIKIA MTU IBADA YA HIJJA

Sharti ni vipengele vya kisheria ambavyo huwa nje ya ibada, kwa maana mja anapotaka kufanya ibada au anapotaka kuingia

katika ibada yoyote ile basi kwanza atalazimika kabla ya kuingia katika ibada hiyo kwa kuitekeleza, itamlazimu kutimiza vipengele hivyo ambavyo vinajuulikana kwa jina la **“SHARTI”** ndipo atakua ameruhusika kuingia ndani ya ibada aliyokusudia kuifanya.
Miongoni mwa sharti ambazo anatakikana mwenye kukusudia kufanya ibada ya Hijja awe amezitimiza ni hizi zifuatazo:-

1) Uisilamu: Kwa hiyo Hijja sio wajibu kwa asiyekua muisilamu, bali haijuzu kwake kuingia mji wa Makka ataamrishwa asilimu kwanza ndipo aruhusiwe kuingia Makka. Dalili ya hayo ni kauli ya Allah (Subahaanahu wata’ala) pale aliposema:

﴿ وَمَن يَبۡتَغِ غَيۡرَ ٱلۡإِسۡلَٰمِ دِينٗا فَلَن يُقۡبَلَ مِنۡهُ وَهُوَ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ ﴾ [آل عِمۡرَان : ٨٥]

“Na yeyote atakaetafuta dini isiyokuwa Uisilamu haitokubaliwa kwake, naye akhera atakua katika wenye kula hasara”.

Kwa hiyo Uisilamu ni sharti katika kukubaliwa matendo ya mja yakiwemo matendo ya ibada ya Hijja, ikiondoka sharti hiyo matendo hayo hayatokubaliwa.

2) Kuwa na akili timamu: Kwa hiyo Hijja sio wajibu kwa mwendawazimu wala haisihi hata akifanya kwa kua yeye muisilamu lakini ikiwa akili haipo timamu.

وَعَن عَلِيِّ بْنِ أَبِي طَالِب رَضِيَ اللهُ عَنْهُ عَنِ النَّبِيِّ ﷺ قَالَ : (رُفِعَ القَلَمُ عَنْ ثَلاَثَةٍ ، عَنِ الْمَجْنُونِ الْمَغْلُوبِ عَلَى عَقْلِه حَتَّى يَبْرَأَ ...) الحَدِيْثُ (رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ وَصَحَّحَهُ الأَلْبَانِيُّ فِي صَحِيْحِ الجَامِعِ : ٣٥١٢).

“Kutoka kwa Aliy bin Abii Twalib (radhiyallahu a’nhu), kutoka kwa Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam) amesema: “Imenyanyuliwa kalamu (kutoandikiwa makosa) kwa watu watatu (katika hao watatu ni) imenyanyuliwa kalamu kwa mwendawazimu aliyezidiwa ikawa akili haifanyi kazi mpaka atakapopona na kuondoka maradhi yake **…**” Hadithi ikaendelea kutaja wengine mpaka mwisho.

3) Kubaleghe: Kwa hiyo Hijja sio wajibu kwa ambae hajabaleghe ingawa akiifanya ibada hiyo itasihi na atapata ujira yule anaempeleka. Ila tu anapobaleghe inampasa afanye Hijja yake tena. Dalili ya hayo ni kauli yake Bwana Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam): pale aliposema:

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ : (رَفَعَتِ امْرَأَةٌ صَبِيًا لَهَا فَقَالَتْ يَا رَسُوْلَ اللهِ أَلِهٰذَا حَجٌّ؟ قَالَ نَعَمْ وَلَكِ أَجْرٌ). (٣٥١٢).

Kutoka kwa Ibnu A’bbas (radhiyallahu a’nhuma), amesema: “Alinyanyua mwanamke mmoja kumnyanyua mtoto mdogo na

Akasema katika hali ya kuuliza: Ewe mjumbe wa Allah je kwa huyu mtoto kuna Hijja? Mtume akasema: Ndiyo, na wewe utapata ujira (malipo)”.

Kwa hiyo mtoto ikiwa atahiji kabla ya kufikia baleghe Hijja yake itasihi na atapata ujira yule aliyemchukua na kumpeleka Makka kuhiji, lakini mtoto huyu akifikia baleghe itamlazimu kuhiji tena kwani atakua ametimiza Sharti.

4) Awe huru wala asiwe mtumwa: Na dalili ya hili ni kutokana na hadithi ya Ibnu ‘Abbas inayosema:

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُوْلُ اللهِ ﷺ: (أَيُّمَا عَبْدٍ حَجَّ ثُمَّ أُعْتِقَ فَعَلَيْهِ أَنْ يَحُجَّ حَجَّةً أُخْرَى). (رَوَاهُ البَيْهَقِيُّ ٥/١٧٩) وَصَحَّحَهُ الأَلْبَانِيُّ فِي صَحِيْحِ الجَامِعِ : ٢٧٢٩).

“Na kutoka kwa Ibnu A’bbas (radhiyallahu a’nhuma), amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam): “Mtumwa yeyote aliyefanya ibada ya Hijja kisha akaachwa huru, basi ni juu yake kufanya ibada ya Hijja nyengine”

Kwa hiyo mwenye kukusudia kufanya ibada ya Hijja asiwe mtumwa, bali awe huru.

5) Awe na uwezo wa kutekeleza ibada yake ya Hijja: Na uwezo hapa umegawika sehemu mbili nazo ni hizi zifuatazo:-
a) Uwezo wa kimali: Kwa maana awe na uwezo wa kimali katika safari yake na awatosheleze atakaowaacha nyuma ambao ni jukumu lake kuwasimamia kimahitaji.

a) Uwezo wa kimwili: Kwa maana awe na afya njema ambayo itakua ni sababu ya kuweza kuitekeleza ibada ya Hijja, afya

njema hiyo ikiambatana na nguvu za kimwili. Dalili ya haya ni aya iliyopo katika Suratu Al-imraan aya nambari 97 ambayo imetangulia katika kipengele cha wajibu wa ibada ya Hijja, na zipo hadithi nyingi sana katika kuelezea sharti hii ila sitozitaja hapa kwa kua sharti ipo wazi pia kwa ajili ya kutorefuka kwa kitabu.

6) Kuwepo maharimu kwa upande wa mwanamke: Sharti hii wanawake wengi wanaikwepa na kutoitimiza imma kwa sababu ya ujinga uliowavaa na kupelekea kuwa mbali na kuisoma dini yao, na hii sio kwa safari ya kuelekea katika ibada ya Hijja tu! Bali safari zote za mbali ni lazima mwanamke asafiri na maharimu wake, lakini leo utakuta mwanamke anasafiri peke yake kuelekea Uturuki, China, Dubai na sehemu nyengine jambo ambalo Uisilamu unalipinga.

وَعَنْ عَبْدِ اللهِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُوْلُ اللهِ ﷺ: (لاَ تُسَافِرُ الْمَرْأَةُ إِلاَّ مَعَ ذِيْ مَحْرَمٍ، وَلاَ يَدْخُلُ عَلَيْهَا رَجُلٌ إِلاَّ وَمَعَهَا مَحْرَمٌ، فَقَالَ رَجُلٌ: يَا رَسُوْلَ الله! إِنِّي أُرِيْدُ أَنْ أَخْرُجَ فِي جَيْشِ كَذَا وَكَذَا وَامْرَأَتِي تُرِيْدُ الْحَجَّ، فَقَالَ اخْرُجْ مَعَهَا). (رَوَاهُ الْبُخَارِيُّ : ١٨٦٢)، (وَمُسْلِم :٣٢٧٢).

“Na kutoka kwa Abdillah Ibnu A’bbas (radhiyallahu a’nhuma) amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam): “Asisafiri mwanamke isipokua asafiri na mahrimu wake, na wala asiingie kwake huyo mwanamke mtu yeyote wa kiume isipokua akuwepo mahrimu wake huyo mwanamke, Basi akasema mtu mmoja: Ewe mjumbe wa Allah! Hakika mimi

nataka nitoke pamoja na jeshi kadha wa kadha (kwenda vitani) na ilhali mke wangu anataka kwenda kuhiji? Akasema Mtume: toka pamoja na mke wako (kwenda kwenye ibada ya Hijja).

Na amesema mwanachuoni Abdul-Muhsin Al-abbadi wakati alipokua akitolea maelezo hadithi hii kwa kauli yake hii:

{ فَقَدْ أَرْشَدَ النَّبِيُّ ﷺ السَّائِلَ فِي هٰذَا الحَدِيْث إِلَى تَرْكِ الجِهَادِ لِيُسَافِرَ مَعَ امْرَأَتِه لِلْحَجِّ، وَلَوْ حَجَّتْ الْمَرْأَةُ بِغَيْرِ مَحْرَمٍ صَحَّ حَجُّهَا وَأَثِمَتْ لِسَفَرِهَا بِدُوْنِ مَحْرَمٍ، لِأَنَّ اشْتِرَاطَ المَحْرَمِ شَرْطُ الوُجُوبِ لاَ لِلصِّحَّةِ } (١)

“Basi kwa hakika Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) amemuongoza muulizaji katika hadithi hii katika jambo la kuacha kwenda kupigana jihadi kwa ajili ya kumruhusu kusafiri na mke wake kwenda kutekeleza ibada ya Hijja, na lau mwanamke atakwenda kuhiji pasi na kufuatana na mahrim wake, Hijja yake itasihi na atapata madhambi ya kusafiri peke yake pasi na mahrimu wake, kwasababu sharti ya mahrimu ni sharti ya wajibu na siyo sharti ya kusihi kwa ibada ya Hijja ”.

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu):

Maharimu wa mwanamke ambao anaweza kufuatana nao wamegawika sehemu tatu, nazo ni hizi zifuatazo:-

---

(١) انظر : ((تبصير الناسك بأحكام المناسك ، ص ٢٧)) للعلامة عبد المحسن العباد

a) Maharimu wa mwanamke, wa mwanzo ni:-

- Mume wake, huyu mi wa mwanzo anaruhusika kufatana nae ikiwa mwanamke ameolewa.

b) Maharimu wa mwanamke, wa pili ni wale wa kinasabu, nao ni hawa wafuatao:-

- Baba yake mwanamke
- Mtoto wake mwanamke
- Kaka yake mwanamke au ndugu yake wa kiume
- Ammi yake (Baba yake mdogo) mwanamke
- Mjomba yake mwanamke

c) Maharimu wa mwanamke, wa tatu ni wale waliyokua maharimu wake baada ya kujitokeza sababu ambazo zilizosababisha kupatikana huo umaharimu, kama vile kunyonya ziwa moja nao ni hawa wafuatao:-

- Baba wa mume wake mwanamke
- Mtoto wa mume wake mwanamke
- Mume wa mama yake mwanamke ambae ameshaingia nae ndani huyo mama mtu
- Mume wa mtoto wake wa kike huyo mwanamke.

  Basi hao ndiyo maharimu wa mwanamke ambao sharia inamruhusu kutoka na yeyote kati ya hawa ili mwanamke awe katika hifadhi na kutofanyiwa maudhi yoyote yale njiani wakati yumo safarini

NASAHA MUHIMU KWA KILA TAASISI YA MAHUJAJI

Kama inavyofahamika kuwa taasisi nyingi sharti hili hawajalitilia umuhimu ni kwa miongoni mwa sababu zifuatazo:-

- Kughafilika kwao na sharti hili na kutolijua kuwa ni sharti la lazima kwa mwanamke wa kiislamu wakati anapotaka kusafiri safari yoyote ile ya mbali kua ni lazima asafiri na maharimu wake.

- Kujua kwao kua sharti hili lipo lakini kupatikana kuzembea na kulidogesha sharti hili na kusema kwao kua wanawake wanaosafiri wapo wengi kwa hiyo watasaidiana wao kwa wao. Kusema kwao huku si sawa na kuna kwenda kinyume na mafundisho ya Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam), na tumeona namna Mtume alivyomtaka yule mtu aliyekusudia kwenda jihadi kua aache kwenda jihadi na ampeleke mke wake Hijja. Kwa hiyo zindukeni enyi ndugu zangu mnaowasimamia mahujaji ili muepukane na dhambi hii ya kusafiri mwanamke bila ya mahrimu wake.

- Baadhi ya taasisi zipo zaidi kuiangalia pesa inayoingia kwao na ikiwa mwanamke hajakamilisha sharti hili la kuwepo mahrimu wake basi hua hawamuelekezi katika hilo bali wao humpokea na kumuingizakatika idadi ya mahujaji watarajiwa, na hili tumeshuhudia wengi katika mahujaji wa kike kusafirishwa na taasisi kwenda kuhiji bila ya maharimu zao. Enyi wasimamizi wa taasisi za mahujaji hebu zingatieni zaidi usahihi wa hii ibada kuliko kuzingatia pesa inayoingia mikononi mwenu zaidi, basi kwa kufanya hivyo itapelekea kuhuwisha Uisilamu katika uhalisia wake na kinyume na hivyo itakua ni kuukandamiza Uisilamu, kwa sababu taasisi zinaona sawa na ni

jambo sahihi mwanamke kusafiri kwenda Hijja bila ya maharimu wake, na Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) anaona si sawa na ndo maana tukasema watu wakienda kinyume na haya ya Mtume watakuwa wanaukandamiza Uisilamu.

NASAHA KWA KILA MWANAMKE ANAYEKUSUDIA KUFANYA IBADA YA HIJJA

Ewe mwanamke wa kiislamu ambae unaefuata Uisilamu wako kama vile alivyofundisha Bwana Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) elewa ya kwamba, Uisilamu umekuthamini na umekuweka katika heshima kubwa na Uisilamu umekufanya wewe ni mfalme ikiwa utazingatia vyema, na Uisilamu umekuwekea utaratibu maalumu wakati utakapokua unataka kusafiri safari ya mbali ni kwamba usisafiri bila ya kuwepo mahrimu wako.

Kwa hiyo popote pale utakapotaka kusafiri basi tafuta katika hao tuliowataja mahrimu yeyote ambae atakaeweza kukamilisha sharti yako hii ili utakaposafiri kwenda kufanya ibada ya Hijja uifanye katika hali nzuri sana bila ya kupata dhambi yoyote ile.

AINA ZA IBADA YA HIJJA

Ibada ya Hijja ina aina zake, nazo ni hizi zifuatazo:-

1) TAMATTUI: Nayo ni haji atahirimia katika miezi ya Hijja kufanya Umra peke yake, anapofika Makka hutufu na kufanya sa'ayi kisha kunyoa nywele, inapofika siku ya Tarwiya

(tarehe nane Dhul-hijja) atahirimia kwa ajili ya Hijja peke yake na kufanya yote yanayompasa kufanya aliye katika Hijja.

2) <u>QIRAAN:</u> Nayo ni kua atahirimia Hijja na Umra pamoja, anapofika Makka hutufu Twawaafu quduum, kisha atafanya sa'ayi baina ya Swafa na Marwa kwa ajili ya Hijja na Umra pamoja, kisha atabaki kaika Ihram mpaka siku ya Iddi ndipo atakapo halalika.

3) <u>IFRAAD:</u> Nayo ni kua atahirimia kwa ajili ya Hijja peke yake atakapofika Makka atatufu Twawaafu quduum, kisha atafanya sa'ayi ya Hijja yake, na atabaki katika Ihram mpaka ahalalike siku ya Iddi na hachinji.

Na aina bora yao katika aina tatu ni aina ya mwanzo nayo ni **TAMATTUI** ambayo Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) amewaamrisha maswahaba zake kuifanya hiyo na kuwahimiza juu yake pale aliposema:

(...أحِلُّوْ مِنْ إحْرَامِكُم بِطَوَافِ البَيْتِ وَبَينَ الصَّفَا وَالمَرْوَةَ وَقَصِّرُوا، ثُمَّ أقِيْمُوا حَلاَلاً حَتَّى إذَا كَانَ يَوْمُ التَّرْوِيَةِ فَأَهِلُّوا بِالْحَجِّ واجْعَلُوا الَّتِي قَدَّمْتُمْ بِهَا مُتْعَةً، فَقَالُوا: كَيْفَ نَجْعَلُهَا مُتْعَةً وَقَدْ سَمَّيْنَا الْحَجَّ؟ فَقَالَ: افْعَلُوا مَا أَمَرْتُكُم فَلَوْلاَ أَنِّي سُقْتُ الهَدْيَ لَفَعَلْتُ مِثْلَ الَّذِي أَمَرْتُكُم، وَلَكِنْ لاَ يَحِلُّ مِنِّي حَرَامٌ حَتَّى يَبْلُغَ الهَدْيُ مَحِلَّهُ فَفَعَلُوا). (رواه البُخَارِيُّ: ١٠٦٨)، (ومُسْلِم: ١٢١٦) مِن حَدِيْثِ جَابِرِ بنِ عَبدِ اللهِ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ

“… Halalikeni (kuweni katika hali ya halali kwa kuvua Ihram na kufanya yale yote wakati wa kua mumevaa Ihram ilikuwa haifai kuyafanya) kwa kutufu nyumba ya Al-qaaba na kwenda sa’ayi baina ya Swafa na Marwa na kupunguza nywele, kisha kaeni hali ya kua mupo halali, mpaka itakapokua siku ya Tarwiya (tarehe nane ya Dhul-hijja) basi mtahirimia Hijja na yafanyeni yale ambayo mliyotangulia nayo kuwa ni matendo ya Umra yanayounganishwa kwenye Hijja, wakasema: Vipi tutafanya kua ni matendo ya Umra yanayounganishwa kwenye Hijja na hali ya kua sisi tumeita na kutamka Hijja (matendo ya Hijja moja kwa moja)? Basi Mtume akasema: Fanyeni nilivyokuamrisheni, basi lau mimi si kuchunga mnyama ningelifanya mfano wa vile nilivyokuamrisheni nyinyi, na lakini si halali kwangu haramu mpaka mnyama wa kuchinjwa atakapofika mahala pake, basi maswahaba wakatekeleza vile walivyoamrishwa na Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam)”.

Kwa hiyo ndio bora yao na ndiyo inayotekelezwa mara nyingi kuliko aina hizo nyengine.

VITUO VYA KUHIRIMIA (MIQAAT)

Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) ameweka vituo (mipaka) vya kuhirimia kwa ajili ya ibada ya Hijja na Umra, na vituo hivyo ni vitano ambavyo Hijja na Umra huhirimiwa kuanzia hapo, navyo ni hivi vifuatavyo:-

a) Kituo cha watu wa Madina na wanaopitia Madina ni Dhul-huleifa hujulikana leo kama AbyaarAli, umbali wake wa mji wa Makka ni 450km.

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu): Amma kisa kinachonasibishwa kuwa pameitwa sehemu hiyo ni AbyaarAli kua sehemu hiyo pana kisima cha swahaba wa Mtume nae ni Aliy bin Abii Twalib na hapo alimuua jinni, hicho ni kisa cha uongo na wala hakijasihi bali ni uongo na hayo wameyaeleza wanawachuoni wakubwa katika vitabu vyao, katika hao ni Sheikh Albaniy (Rahmatullah a'layhi) ameleza katika kitabu chake alichokiita kwa jina la (Manaasikul hajji wal-umra fil kitabu wasunna wa aatharussalaf) katika ukurasa wa 14.

b) Kituo cha watu wa Sham, Misri na Morocco na wale wanaopita njia yao ni Juhfa iliyopo karibu na mji wa Raabigh na watu huhirimia leo kutoka Raabigh umbali wake na mji wa Makka ni 183km.

c) Kituo cha watu wa Najdi na wale wanaopitia huko ni Qarnul-manaazil, na leo huitwa Asseilul-kabiir, umbali wake na mji wa Makka ni 75km.

d) Kituo cha watu wa Yemen na wanaopitia huko ni Yalamlam, na leo watu huhirimia sehemu inayoitwa Sa'diyya, umbali wake na mji wa Makka ni 92km.

e) Kituo cha watu wa Iraaq na wanaopitia huko ni Dhaatu-I'rqi, umbali wake na mji wa Makka ni 94 km.

Na dalili iliyokuja kutaja vituo hivyo ni hadithi ya Abdillah bin Abbas (radhiyallahu 'anhu) inavyosema hivi ifuatavyo:-

وَعَنْ عَبْدِ اللهِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ: (وَقَّتَ رَسُوْلُ اللهِ ﷺ لِأَهْلِ المَدِيْنَةِ ذَا الحُلَيْفَةَ، وَلِأَهْلِ الشَّامِ الجُحْفَةَ، وَلِأَهْلِ نَجْدٍ قَرْنَ المَنَازِلِ، وَلِأَهْلِ الْيَمَنِ يَلَمْلَمَ، فَهُنَّ لَهُنَّ وَلِمَنْ أَتَى عَلَيْهِنَّ مِنْ غَيْرِ أَهْلِهِنَّ لِمَنْ كَانَ يُرِيْدُ الحَجَّ وَالعُمْرَةَ، فَمَنْ كَانَ دُوْنَهُنَّ فَمُهَلُّهُ مِنْ أَهْلِهِ وَكَذَلِكَ حَتَّى أَهْلُ مَكَّةَ يُهِلُّوْنَ مِنْهَا). (رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ٠٤١٥)، (وَمُسْلِم: ١١٨١).

Na kutoka kwa Abdillah Ibnu A’bbas (radhiyallahu a’nhuma) amesema: “Ameweka Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) mipaka (vituo) na amewaekea watu wa Madina kituo cha Dhul-hulaifa, na kwa ajili ya watu wa Sham kituo cha Juhfa, na kwa ajili ya watu wa Najdi ni kituo cha Qarnul-manaazil, na kwa ajili ya watu wa Yemen ni kituo cha Yalamlam, na kwa ajili ya wale watakaopita sehemu hizo kwa wale wasiokua watu wa sehemu hizo, ni kwa ajili ya yule anaetaka na kukusudia kufanya ibada ya Hijja na Umra, basi wale walio karibu na mji wa Makka kuhirimia kwao ni kwa watu wake hizo sehemu na vile vile kwa watu wa Makka watahirimia kupitia hiyo Makka”

Na kuhusu watu wa Iraq kituo chao kimetajwa katika tamko hili lifuatalo:-

وَقَـــالَ عَبدُ اللهِ بنُ عُمَرَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا: حَدَّثَنِي أَصْحَابُنَا (أَنَّ رَسُولَ اللهِ ﷺ وَقّتَ لِأَهْلِ العِرَاقِ ذَاتَ عِرْقٍ). (رَوَاهُ أَبُو نُعَيْمٍ فِي حِلْيَةِ الأَوْلِيَاءِ : ٤/٩٧)

Na amesema Abdillah Ibnu Omar (radhiyallahu a'nhuma): Na wamenihadithia mimi watu wetu ya kwamba "Hakika Mtume wa Allah (Swallallahu a'layhi wasallam) amewaekea kituo watu wa Iraq kinachoitwa Dhaatu Irqi".

Ni wajibu kwa kila anaepita katika hivi vituo akiwa na nia ya kufanya Hijja au Umra ahirimie kutoka hapo, iwapo atapita katika hivyo vituo bila ya kuhirimia hakuna budi atalazimika kurudi tena ili ahirimie katika kituo husika, na iwapo hatarudi akahirimia baada ya kukipita kituo cha kuhirimia basi atalazimika kuchinja.

MATENDO YA MWENYE KUTAKA KUFANYA UMRA AU HIJJA KATIKA VITUO VYA KUHIRIMIA

Matendo ya mwenye kutaka kufanya Umra au Hijja katika vituo vya kuhirimia ni haya yafuatayo:-

1. Panapendezeshwa kwa yule aliyekusudia kufanya ibada ya Hijja na Umra kuoga kwa ajili ya Ihram hata kama ni mwanamke aliyekua katika ada (hedhi) ya mwezi au damu ya uzazi.

2. Ni sunna kujipaka manukato mazuri yenye harufu nzuri mwilini, katika ndevu na nywele kwa mwanamme, isipokuwa wanawake wao watajitia manukato yasiyokua na harufu. Na haya ya kujitia manukato ni kabla ya kunuwiya kuvaa Ihram baada ya kuoga, yaani baada ya kuoga na kabla ya kunuwiya Ihram, na amma baada ya kuvaa Ihram pamoja na nia ndiyo mtu akataka kujitia manukato ni haramu.

3. Atanyoa na kuondoa kila alichoruhusiwa kukikata, kama vile sharubu na kusafisha sehemu za siri na kila anachokihitaji kukiondoa katika mwili wake, na kitendo hiki hakihusu Ihram ila ni kwasababu asije akahitaji kujisafisha baada ya Ihram na hapo itakua ni haramu kwake, ama ndevu ni haramau kuzinyoa kabla na baada ya Ihram, bali katika nyakati zote ni haramu kunyoa ndevu.

NASAHA KWA MAHUJAJI JUU YA JAMBO LA KUNYOA NDEVU

Enyi ndugu zangu fahamuni kua kunyoa ndevu haifai, na mtu akinyoa ndevu anakua amekhalifu amri ya Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) kwani Mtume anakuamrisha kua ndevu usizinyoe na wewe unazinyoa kwa makusudi, huko ni kumpinga Bwana Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam).

(أَحْفُوا الشَّوَارِبَ وَأَعْفُوا اللِّحَى). مِنْ حَدِيثِ ابنِ عُمَرَ وَأَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا، أَوْرَدَهُ العَلاَّمَةُ الأَلبَانِي فِي صَحِيحِ الجَامِعِ بِرَقْمِ ٢٠٧ وَصَحَّحَهُ.

"Punguzeni masharubu na ziachilieni (kwa maana msiziguse na mkataka kuzinyoa ndevu)"

Ndevu hazinyolewi bali zinaachiwa ziwe kubwa na wala sio katika kuzitunza ndevu kwa kule kuzipunguza au kuzinyoa bali kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mafundisho ya Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam).

Sasa ewe mwenye kufanya ibada ya Hijja epuka na kosa hili la kunyoa ndevu sawa ukiwa upo Makka au umerudi Makka kwani kunyoa ndevu ni haramu, basi epuka haramu ili upendwe na Allah na Mtume wake.

4. Kisha kwa mwanamme atavaa izari na ridaa (shuka ya juu na shuka ya chini) yapendekezwa zaidi ziwe nyeupe na safi, ingawa sio sharti ya kua lazima ziwe nyeupe bali yajuzu kuvaa rangi nyengine yoyote.

TANBIHI: Wengi wa watu wanaona ni sharti au lazima kuvaa nguo nyeupe, bali nyengine pia zinafaa ikiwa mtu hakupata nyeupe, kinachokusudiwa ni kupatikana mashuka mawili, la juu ambalo linajuulikana kwa jina la **RIDAA** na shuka la chini linajuulikana kwa jina la **IZAARI**. Bali mashuka meupe na nguo nyeupe ndo zinazopendekezwa kuvaa lakini sio lazima, na dalili ya haya ni hadithi ifuatayo:-

وَعَنْ عَبْدِ اللهِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُوْلُ اللهِ ﷺ: (اِلْبَسُوْا مِن ثِيَابِكُم البَيَاضَ فَإِنَّهَا مِنْ خَيْرِ ثِيَابِكُم، وَكَفِّنُوا فِيْهَا مَوتَاكُمْ). الحَدِيْث

(رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ فِي سُنَنِهِ : ٣٨٧٨)، وَصَحَّحَهُ الأَلبَانِي فِي صَحِيْحِ الجَامِعِ بِرَقْمِ (١٢٣٦)، وأَحْمَد شَاكِر فِي تَخْرِيْجِ مُسْنَدِ أَحْمَدَ (٤٨/٤)، وَشُعَيبُ الأَرْنَاؤُوطِ فِي تَخْرِيْجِ صَحِيْحِ ابن حِبَّانٍ بِرَقْمِ (٥٤٢٣).

“Na kutoka kwa Abdillah Ibnu A’bbas (radhiyallahu a’nhuma) amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam): “Vaeni katika nguo zenu nyeupe kwa sababu hizo nguo nyeupe ni bora ya nguo zenu, na wakafinieni (wavikeni sanda) maiti zenu hizo nguo nyeupe”.

Hii hadithi inaonesha wazi kua nguo nyeupe zinapendekezwa kuvaliwa zaidi, lakini pia hadithi inajuulisha kua kuvaa nguo nyengine inafaa na wala hakuna ubaya wowote ule. Kwa hiyo wazinduke wale wanaodhania kua nguo za Hijja na Umra ni ihram nyeupe, na endapo mtu akionekana amevaa shuka ya ihram ya rangi isiyokua nyeupe humdhania kuwa amekosea kukubwa.

Basi jambo haliko hivyo mnavyodhania, fahamu hili kwa elimu sahihi na siyo dhana.

5. Anaruhusika kwa mwenye kuhirimia kuvaa Ihram yake kutoka nyumbani kwake, kama alivyofanya Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) na swahaba zake, na jambo hili humfanyia wepesi zaidi yule anaesafiri kwa ndege, kwa sababu ni uzito kuvaa akiwa juu ya ndege kwa hiyo itajuzu kwao kupanda ndege wakiwa na vazi la Ihram, lakini hawatahirimia hadi wakaribie au wafike katika vituo vya kuhirimia.

MAELEZO YA ZIADA: Ikiwa itawezekana kwa taasisi za mahujaji kutoka mapema yaani kufika mapema katika miji mitakatifu ya Makka na Madina katika Hoteli zao walizozikodi, ni nyema kufanya hivyo, na ikifika siku ya kuanza ibada ya Hijja na Umra inakua ni rahisi wao mahujaji kuvaa nguo zao wakiwa hotelini, na pia inakua ni rahisi kwenda kwenye kituo

cha kuhirimia, hususan kwa wale watakaofika mapema katika mji wa Madina wakipata kituo cha Dhul-hulaifa ambapo alihirimia Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) na swahaba zake.

6. Ihraam haina swala maalumu, ila ikisadifiana na swala basi ataswali swala yake ya faradhi kisha aingie katika Ihram, ikiwa sio wakati wa swala ya faradhi basi ataswali rakaa mbili kwa nia ya sunna ya udhu, kwa mwanamke aliye katika ada ya mwezi (hedhi) au damu ya nifasi basi yeye hatoswali.

TANBIHI: Kwa wale mahujaji watakao anzia mji mtukufu wa Madina, wao watasali rakaa mbili za udhu wakiwa hotelini, na wakifika katika kituo cha kuhirimia ambacho ni Dhul-hulaifa watasali rakaa mbili za sunna ya hiyo sehemu kwa utukufu wake (hiyo sehemu), na sunna hiyo sio kwa ajili ya Ihram kama wanavyodhania baadhi ya watu, bali rakaa mbili hizo ni kwa ajili ya utukufu wa hiyo sehemu. Dalili ya hayo ni hadithi ya Bwana Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) inayosema:-

وَعَن عُمَرَ بنِ الخَطَّابِ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُوْلَ الله ﷺ بِوَادِي العَقِيْقِ يَقُولُ: (أَتَانِي اللَّيْلَةَ آتٍ مِنْ رَبِّي فَقَالَ: صَلِّ فِي هَذَا الوَادِيْ المُبَارَكِ، وَقُلْ عُمْرَةً فِي حَجَّةٍ). (رَوَاهُ البُخَارِيُّ ٧٣٤٣)

"Na kutoka kwa Omar Ibnu Khatwab (radhiyallahu a'nhu), amesema: Nimemsikia Mtume wa Allah (Swallallahu a'layhi wasallam) akiwa katika bonde la Al-'akiki akisema: "Amenijia aliyenijia (ambae huyo aliyekuja kwa Mtume ni Jibril kama

alivyotajwa katika riwaya nyengine kwa uwazi) kutoka kwa Mola wangu na akasema: “Swali katika bonde hili lenye Baraka na lililobarikiwa, na sema U’mra ndani ya Hijja (katika baadhi ya riwaya) U’mra na Hijja.

Je! mtu ikiwa amefika sehemu hiyo na hana udhu akenda kutia udhu, anaruhusika kuswali rakaa mbili za udhu na rakaa mbili za utukufu wa hiyo sehemu?

Jawabu: Anaruhusika kuswali rakaa mbili za udhu na rakaa mbili za utukufu wa hiyo sehemu, ila kilicho bora kwa hujaji awe ametoka na udhu hotelini alipofikia na ni vyema rakaa mbili za udhu aziswali akiwa hotelini ndo inahesabika kama nyumbani alipo kwa kipindi hicho, na akifika katika kituo hicho cha kuhirimia ataswali na kuhirimia.

Kwa hiyo lifahamike hili kua hakuna swala ya Ihram bali kwa kituo cha watu wa Madina ambacho ni Dhul-hulaifa kuna sunna ya kuswali hapo, lakini vituo vilivyobakia hakuna sunna ya kuswali katika vituo hivyo, isipokua itakaposadifu swala imma swala ya faradhi au swala ya sunna, kama vile rakaa mbili za udhu hapo ndo zitaswaliwa rakaa mbili hizo.

7. Baada ya kumaliza kuswali atahirimia (na hii ni kwa wale waliyo katika vituo vya kuhirimia) na Ihram ni nia ya kuanza matendo ya Hijja na U’mra atanuwiya kwa moyo wake aina ya Hijja anayotaka kuitekeleza au atanuwiya Umra ikiwa ni Umra, na hapa atatamka kile alichokinuwiya ikiwa ni Tamatui atasema:

((لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ بِعُمْرَةٍ))[1]

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

“Labbaika llaahumma bi U’mra”

8. Kuanzia hapo atakuwa ameingia katika ibada yake, hapo ataanza kuleta Talbiya, nayo ni kusema:

((لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لاَ شَرِيْكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الْحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالْمُلْكُ، لاَ شَرِيْكَ لَكَ)).

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

“Labbaika llahumma labbaika, labbaika laa sharika laka labbaika, Innal hamda wanneamata laka walmulku, laa sharika laka”

9. Anaamrishwa anayeleta Talbiya awe ananyanyua sauti yake Kwa sababu ndivyo alivyoamrisha Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) katika hadithi ifuatayo:-

---

1. Panapendezeshwa baada ya kunuwia kusema kama ifuatavyo:
((اللَّهُمَّ هَذِهِ حِجَّةٌ لاَ رِيَاءَ فِيْهَا وَلاَ سُمْعَةً))
“Allahumma haadhihi hijjatun laa riyaa walaa sum-atan”

وَعَنِ السَّائِبِ بْنِ خَلاَّدٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: سَمِعْتُ رَسُوْلَ اللهِ ﷺ بِوَادِي العَقِيْقِ يَقُولُ: (أَتَانِي جِبْرِيْلُ فَأَمَرَنِي أَنْ آمُرَ أَصْحَابِيْ وَمَنْ مَعِيْ أَنْ يَرْفَعُوا أَصْوَاتَهُم بِالتَّلْبِيَـــةِ). (رَوَاهُ أَصْحَابُ السُّنَنِ وَغَيْرُهُم وَصَحَّحَهُ الأَلبَانِي فِي صَحِيْحِ أَبِي دَاوُدَ بِرَقْمِ (١٥٩٢).

“Na kutoka kwa Assaaibu Ibnu Khalladu (radhiyallahu a’nhu), amesema: Nimemsikia Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam) akisema: “Amenijia Jibril na akaniamrisha ya kwamba niwaamrishe swahaba zangu (maswahaba zangu) na wale walio pamoja na mimi, kunyanyua sauti zao wakati wanapotamka Talbiya”

Kwa hiyo kunyanyua sauti ndivyo itakiwavyo wakati mahujaji wanapotamka Talbiya na sio kutamka kidogo kidogo au kimya kimya.

10. Wanawake pia ni kama wanaume katika hili, watanyanyua sauti zao, na dalili ya hili ni hadithi ya Assaaibu Ibnu Khalladu ambayo ndani yake kuna maneno yanayosema “na wale walio pamoja na mimi, walio pamoja na Mtume ni wengi wakiwemo wake zake na wanawake wengine katika wake wa maswahaba zake.

NASAHA KWA WANAWAKE MAHUJAJI

Wanawake mahujaji sauti zao wasizipambe na kuziregeza kwa ajili ya kuwatia fitna wanaume, kwani kufanya hivyo ni kuingia makosani kwa makusudi, jambo ambalo litatia mapungufu ibada

yako ya Hijja, basi zinduka ewe hujaji wa kike na epukana na kila fitna na shari kiujumla wake. Pia sauti zao wanawake watazishusha itakapokua karibu yao wapo wanaume ili kujiepusha na fitna ya kuwafitinisha wanaume.

11. Mahujaji watalazimiana na kuendelea kuleta na kutamka Talbiya muda wote watakapokua wapo njiani kuelekea Makka, kwa sababu ni katika alama kubwa za Hijja.

12. Hujaji atakapofika mji wa Makka na akiona majumba ya Makka hapo ataikata Talbiya hiyo ili kujishughulisha na yanayofuata katika ibada yake ya Hijja.

MAMBO AMBAYO SI KATIKA MAKOSA KWA MUHRIM (ALIYE KATIKA HIJJA NA U'MRA) KUYAFANYA

Ni jambo la muhimu kwa kila mlinganizi awe atalazimiana na kuwafanyia watu wepesi katika ibada zao kwa ujumla na mahujaji khaaswa, kwa sababu wepesi na usahali ni katika misingi ya sharia yetu ya Kiisilamu tukufu, kama inavyojuulikana maadamu wepesi huo hautakhalifu Qur-ani na wala Sunna, amma inapokuja dalili basi hapo hamuna nafasi ya kutumia rai wala fikira ya mtu.

Na huu ndio msimamo wa kati na kati ambao ni wajibu wa mlinganizi kushikamana nao wala asizingatie, baada ya hapo atakaesema katika watu kwa sababu ya kua kwao kinyume na yeye ya kua amechupa mipaka na mkali sana au amezembea.

Mambo yanayojuzu kwa Muhrim kuyafanya ingawa wengi katika mahujaji huyaona ni makosa, kwa sababu ya fatwa

zinazotolewa na wale wasioshikamana na msingi tuliotaja hapo juu, nimeonelea nitanabahishe na kuyataja mambo hayo, nayo ni haya yafuatayo:-

1. Kuoga kwa Muhrim hata akisugua kichwa chake, hilo limethibiti kwa Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) katika Sahihi Bukhari na Muslim na wengineo kutokana na hadithi ya Abuu Ayyubu (radhiyallahu a'nhu).

2. Kujikuna kichwa hata zikianguka baadhi ya nywele, kwa ushahidi wa hadithi ya Abuu Ayyubu tuliyoiashiria hapo punde, na hili ndio chaguo la Sheikhul-Islaam (Allah amrehemu).

3. Kunusa harufu nzuri kama vile waridi na kadhalika na kutoa kucha iliyovunjika.

4. Kujifunika na kivuli cha mwavuli, hema au ndani, amma kile kinachofanywa na baadhi ya makundi mapotevu kuondoa kwa Saqfu ya (paa la) gari na kuifanya gari juu ipo wazi eti kwa kufanya kwao huku wanaepuka kujifunika kichwani, huku ni kufanya uzito usiyokua na faida yoyote, na uzito huu ndio uliokatazwa katika dini kwani dini ni nyepesi na hatoleta uzito yoyote yule katika dini isipokua itamshinda kwa sababu ya huo uzito aliouleta katika dini.

5. Kuvaa ukanda kiunoni, kuvaa pete pia, yote hayahayakukatazwa, pia kuvaa miwani iwe ni ya jua au ya macho, kuvaa saa ya mkono, kubeba kipochi cha pesa na vitu vya muhimu shingoni.

6. Kuoga kwa kutumia sabuni yenye harufu kwa sababu si manukato, wala haambiwi anaetumia (amejipaka) manukato na asipotumia ni bora.

7. Yajuzu kwa mwanamke kutumia tembe (dawa) za kuzuia ada yake ya mwezi katika Hijja na Umra, ikiwa hazitamletea madhara (kwa sharti ya kutopatikana madhara katika mzunguko wake wa ada yake na madhara mengine, na hayo ni kwa uthibitisho wa madaktari bingwa).

8. Kuuwa mnyama na wadudu wenye kumuudhi mwanadamu kama panya na kadhalika.

9. Yajuzu kwa mwanamke Muhrim (aliye katika Hijja na Umra) kusoma Qur-ani hata katika ada yake ya mwezi, na hii ndio kauli yenye nguvu katika mas-ala haya.

10. Yajuzu kwa mwanamke kuhirimia hata akiwa amevaa dhahabu mkononi.

Haya yote yanaingia katika ule msingi tuliyoutanguliza kuutaja hapo juu, ni katika wepesi una usahali wa dini yetu na Allah anaseme:

﴿ يُرِيدُ ٱللَّهُ بِكُمُ ٱلۡيُسۡرَ وَلَا يُرِيدُ بِكُمُ ٱلۡعُسۡرَ ﴾ [البَقَرَة: ١٨٥]

“Allah anakutakieni wepesi na wala hakutakieni uzito”

MAMBO AMBAYO YAMEHARAMISHWA KWA MUHRIM KUYAFANYA

Na afahamu mwenye kuhirimia ya kua, baada ya kuhirimia katika kituo chake alichohirimia kuna mambo ambayo hatakikani kuyafanya, mambo yenyewe ni haya yafuatayo:-

1. Kupunguza sehemu ya nywele, ingawa zikianguka bila ya Kukusudia au akatoa sehemu katika nywele kwa kusahau hakuna tatizo, dalili ya hayo ni kauli yake Allah (Subhaanahu wata'ala) pale aliposema:

﴿ وَلَا تَحۡلِقُواْ رُءُوسَكُمۡ حَتَّىٰ يَبۡلُغَ ٱلۡهَدۡيُ مَحِلَّهُۥۚ فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوۡ بِهِۦٓ أَذٗى مِّن رَّأۡسِهِۦ فَفِدۡيَةٞ مِّن صِيَامٍ أَوۡ صَدَقَةٍ أَوۡ نُسُكٖۚ ﴾ [البَقَرَة : ١٩٦]

"Wala msinyoe vichwa vyenu mpaka wanyama hoa wafike machinjioni mwao, na atakaekuwa mgonjwa au ana vya kumuudhi kichwani mwake basi atoe fidia kwa kufunga au kwa kutoa sadaka au kuchinja wanyama"

Kwa hiyo kupunguza au kunyoa nywele wakati ushaingia kwenye Ihram ni jambo lisilofaa, lifahamu hili ewe hujaji.

2. Kupunguza kucha (kukata kucha) isipokua kucha imekatika wenyewe anaruhusiwa kuondosha hiyo iliyokatika.

[أَجْمَعَ أَهْلُ العِلْمِ عَلَى أَنَّ المُحْرِمَ لاَ يَجوْزُ لَهُ قَلْمُ أَظَافِرِهِ وَأَجْمَعُوا أَيْضًا عَلَى أَنَّ المُحْرِمَ أَنْ يُزِيْلَ ظَفْرَهُ إِذَا انْكَسَرَ] (المُغْنِي : ١٤٦/٥)

(الإِقنَاعُ مِنْ مَسَائِلِ الإِجْمَاعِ : ٧٦/١) .

“Wamekubaliana watu wa elimu (wanachuoni) juu ya kwamba Muhrim haijuzu kwake yeye kukata kucha zake na wamekubaliana vile vile kua anayoruhusa Muhrim kuondosha kucha yake iliyokatika.

وَعَنِ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: (المُحْرِمُ يَدْخُلُ الْحَمَّـامَ، وَيَنْزِعُ ضِرْسَهُ، وَيَشُمَّ الرَّيْحَانَ، وَإِذَا نْكَسَرَ ظُفْرُهُ طَرَحَهُ، وَيَقُولُ: أَمِيطُوا عَنْكُمُ الأَذَى، فَإِنَّ اللهَ عَزَّ وَجَلَّ لاَ يَصْنَعُ بِأَذَاكُمْ شَيْئًا). (رَوَاهُ البَيْهَقِيُّ فِي سُنَنِهِ ٦٨٩٠) وَصَحَّحَهُ الأَلْبَانِيُّ فِي حَجَّةِ النَّبِيِّ ﷺ : ٢٨ و ٢٩).

“Na kutoka kwa Ibnu A’bbas (radhiyallahu a’nhuma), amesema: “Muhrim anaruhusika kuingia chooni (kwa ajili ya kukoga) na kung’oa jino lake, na kunusa harufu nzuri, na kucha itakapokatika anaruhusika kuiondoa, (Ibnu A’bbas) akisema: “Jiondosheeni mambo yanayokuleteeni maudhi, kwa hakika Allah a’zza wajalla hafanyi kwa yale yanayokuleteeni maudhi chochote”.

Kwa maana kukata kucha kwa makusudi haifai isipokua itakapokua kucha imekatika wenyewe basi wewe unaruhusika kuimalizia, ikiwa imekatika na imening’inia unaruhusika kuiondoa ili isikuletee maudhi na mfano wa hilo pia kama vile jino n.k.

3. Haijuzu kwa Muhrim kujitia manukato katika nguo wala mwili wake, ama athari iliyobakia ya manukato aliyojitia kabla

ya Ihram athari hiyo haidhuru. Dalili ya hayo ni hadithi hii ifuatayo:-

وَعَنْ يَعْلَى بْنِ أُمَـيَّةَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ (أَنَّ أَعْرَابِيًّا جَاءَ النَّبِيَّ ﷺ بِالجُعِرَّانَةِ وَعَلَيْهِ جُبَّةٌ وَهُوَ مُتَضَمِّخٌ بِطِيبٍ فَقَالَ: يَا رَسُولَ اللهِ كَيْفَ تَرى فِي أَنْ أُحْرِمَ بِعُمْرَةٍ فِي جُبَّةٍ بَعْدَ مَا تَمَضَّخَ بِالطِّيبِ؟ فَقَالَ: أَمَّا الطِّيبُ الَّذِي بِكَ فَاغْسِلْهُ ثَلَاثَ مَرَّاتٍ وَأَمَّا الجُبَّةُ فَانْزَعْهَا ثُمَّ اصْنَعْ فِي عُمْرَتِكَ كَمَا تَصْنَعُ فِي حَجِّكَ).

(رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ٤٣٢٩)، (وَمُسْلِم: ٢٧٩٨)

Na kutoka kwa Ya’ala bin Umayya (radhiyallahu a’nhu) “Hakika bedui alikuja kwa Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) katika sehemu za Juu’raanah na juu yake amevaa juba hali ya kua amejipaka manukato akasema: Ewe Mtume wa Allah vipi unaona (nipe khabari) kuhusu mtu aliyehirimia Umra katika wakati ambapo tayari amejipaka manukato basi akasema Mtume: Amma kuhusu manukato ambayo yapo kwako basi ikoshe nguo hiyo mara tatu, na amma kuhusu juba livue kisha fanya katika Umra yako kama unavyofanya katika Hijja yako”.

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu): “hadithi zimekuja nyingi sana kuhusu katazo la kua Muhrim haifai kujitia manukato wakati tayari amekwisha hirimia, na kwa maana hii wanasema wanachuoni hivi ifuatavyo:-

[وَهَذِهِ الأَحَادِيْثُ تَدُلُّ عَلَى أَنَّ المُحْرِمَ لاَ يَسْتَعْمِلُ الطِّيْبَ فِي حَالِ إِحْرَامِهِ، لأَنَّهُ مِنَ التَّرَفِ وَلَهُ قَبْلَ الإِحْرَامِ أَنْ يَسْتَعْمِلَ الطِّيْبَ فِي بَدَنِهِ دُوْنَ لِبَاسِهِ، وَلاَ يَضُرُّ بَقَاءُ ذَلِكَ بَعْدَ إِحْرَامِهِ]

Na hizi hadithi zinajuulisha juu ya kwamba Muhrim haifai kutumia manukato katika hali ya Ihram yake, kwa sababu jambo hilo linaharibu Ihram yake, na anaruhusika kutumia manukato kabla ya Ihram kwa kupaka katika mwili wake pasi na mavazi yake na wala haitomdhuru athari iliyobakia baada ya kuhirimia.

4. Haijuzu (haifai) kwa Muhrim mwanamme kujifunika kichwa kwa kinachoshika kichwa kama kutumia Ihram yake, kofia, kilemba, au kuna aina za miamvuli ambayo huvaliwa kichwani pia haifai isipokua ule wa kushika mkononi ndio unaofaa, kwa hiyo zinduka ewe mwenye kufanya ibada ya Hijja usije waona watu wamevaa miamvuli kichwani nawe ukaona inafaa unununwe, jambo hilo si sawa, dalili yake ni kauli ya Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) aliposema:

(لاَ يَلْبَسُ المُحْرِمُ القَمِيْصَ وَلاَ العَمَائِمَ وَلاَ البُرْنُسَ...) الحَدِيْثُ (رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ٥٨٠٢)، (وَمُسْلِم :١١٧٧) مِن حَدِيْثِ جَابِرِ بنِ عَبدِ اللهِ بن عُمَرَ وَاللَّفظُ لِمُسْلِمٍ

"Muhrim haruhusiki kuvaa kanzu, na wala kuvaa kilemba, na wala kuvaa kofia"

FAAIDA: Je, ikiwa amefunika kichwa chake kwa kusahau atafanyaje?

JAWABU: Ni kuondosha hicho alichotumia kufunika kichwa chake pale anapokumbuka na ibada yake itakua sahihi na wala hatolazimika chochote kama vile kuchinja kwa kutoa fidia n.k.

5. Haifai kwa mwanamme kuvaa nguo zilizoshoneshwa (zilizoshonwa) kwa kadri ya viungo (makhiit), nazo ni nguo zinazovaliwa kawaida kama vile kanzu, suruali n.k, uthibitisho wa hayo ni hadithi ya Abdillah Ibn Omar ambayo imetangulia kabla kuingia jambo hili la tano, ndani ya hadithi hiyo kuna katazo kwa Muhrim kuvaa kanzu na suruali.

6. Ni haramu kuwinda mnyama au kusababisha kuwindwa mnyama au pia kusaidia kuwinda kwa kuonesha alipo mnyama huyo au kuonyesha njia ya kufikia wanyama walipo n.k. Dalili ya hayo ni kauli yake Allah (Subhaanahu wata'ala) aliposema:

﴿ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقۡتُلُواْ ٱلصَّيۡدَ وَأَنتُمۡ حُرُمٞ ﴾ [المَائِـدَة : ٩٥]

"Enyi mlioamini, msiue wanyama wa kuwinda nanyi mumehirimia katika Hijja. [Suratul Maaida: 95].

Na akasema tena Allah (Subhaanahu wata'ala):

﴿ وَحُرِّمَ عَلَيۡكُمۡ صَيۡدُ ٱلۡبَرِّ مَا دُمۡتُمۡ حُرُمٗا ... ﴾ [المَائِـدَة : ٩٦]

"Na mumeharamishwa mawindo ya wanayma wa bara madamu (kwa muda wote) mutakao kuwa mumehirimia hijja" [Suratul – Maidah: 96]

7. Haifai na ni haramu kwa Muhrim kuoa au kuolewa akiwa katika hali ya ihram, pia haifai kumuozesha aliye na mamlaka ya kumuozesha kama binti yake, kuposa pia hairuhusiwi. Dalili ya hayo ni Hadithi ya U'thmaan bin A'ffaan (Radhiyallahu a'nhu) amesema: Amesema Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) :

(لاَ يَنْكِحُ المُحْرِمُ وَلاَ يُنْكَحُ ولاَ يَخْطُبُ) الحَدِيْثُ (رواه البُخَارِيُّ : ١٤٠٩)، (ومُسْلِم :١٨٤١) مِن حَدِيْثِ عُثْمَانَ بنِ عَفَّانَ وَ اللَّفظُ لِمُسْلِمٍ.

Haifai (hairuhusiwi) Muhrim kuoa, na wala kuozeshwa na wala kuposa"

FAAIDA: Je ikiwa amefanya jambo hilo la kuoa Yule aliyehirimia (Muhrim) hali ya kuwa hajui au hali ya kughafilika ndoa hiyo ni sahihi?

JAWABU: Jawabu lake ni lile walilolitoa wanachuoni akiwemo mwanachuoni Abdul – Muhsin Al – Abbaad (hafidhwahullahu) kwa kauli ifuatayo:

[وَإِذَا وَقَعَ الْعَقْدُ مِنْ مُحْرِمٍ لَمْ يَصِحَّ، وَهُوَ نِكَاحُ شُبْهَةٍ، وَإِذَا أُرِيْدَ اسْتِمْرَارُ النِّكَاحِ يُجَدَّدُ الْعَقْدُ].

"Na itakapotokea kifungo cha ndoa kwa muhrim ndoa hiyo haitosihi, na ndoa hiyo ni ndoa ya shubha, na ikitakiwa kua ni ndoa yenye kuendelea hapo mbele italazimika ifungwe upya"

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu):
"Maana ya maneno ya mwanachuoni huyu ni kuwa ndoa hiyo ni batili na isiyofaa na ikiwa wataingiliana kwa ndoa hiyo

watakuwa wanazini, sasa ikiwa wataelimishwa na wakajua ni ndoa isiyofaa na wanataka kuwa wanandoa halali hasa baada ya kuhalalika (kuvua ihram zao kwa kuruhusiwa na sheria) itawalazimu ndoa hiyo kufungwa upya ili ipate kusihi na kuwa ndoa ya halali inayokubaliwa na Uislamu”

8. Haifai na ni haramu kwa muhrim kumuingilia mkewe kabla ya kuhalalika au mke akataka na kumrairai mumewe amuingilie pia ni haramu na haifai. Na akifanya kitendo cha jimai (kumuingilia mkewe) kabla ya kuhalalika hijja yake itabatilika na atalazimika kuitimiza mpaka mwisho na itambidi arudi tena mwaka mwengine kufanya Hijja na pia atatoa fidya kuchinja ngamia au ng’ombe yeye na mkewe na ni wajibu (lazima) watubie kutokana na dhambi yao hiyo.

Amma ikiwa kitendo cha jimai (Tendo la ndoa) alilifanya baada ya kuhalalika kwa kwanza (Baada ya kutupa vijiwe katika Jamratul-Alqaaba) na kunyoa kabla ya Twawaaful-ifaadhwah) hapo hijja yake ni sahihi na ni juu yake kuchinja [1].

Amesema Allah (Subhaanahuu Wata’ala):

﴿ٱلۡحَجُّ أَشۡهُرٞ مَّعۡلُومَٰتٞۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلۡحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلۡحَجِّۗ﴾ [البَقَرَة : ١٩٧].

---

1) Maelezo haya yote yapo kwenye athari ya Amru bin Shua’ibu kuoka kwa baba yake, athari ambayo ameisimulia Imam Hakim katika Mustadrak yake (2/65) na Imam Bayhaqiy katika sunani yake (5/167).

“Hijja ni miezi maalum (inajulikana) yoyote aliyekusudia kufanya hijja katika mezi hiyo basi asiseme maneno machafu, wala asifanye vitendo vichafu wala asibishane katika hijja”

Nimesema hapa: “Tamko lililokuja katika aya hii الرفث tamko hili wapo wanachuoni waliotafsiri kuwa ni maneno machafu na wapo waliotafsiri ni tendo la jimai kwa hiyo ni dalili inayoonesha kuwa haifai tendo la ndoa (Jimai) wakati mtu yupo kwenye ihram yake.

9. Ni haram na haifai pia kumkaribia mkewe kwa vitangulizi vya ndoa kama kumbusu n.k.

NAMNA YA KUFANYA U’MRAH

TWAWAAF YA U’MRAH

1) Anapofika mji mtukufu wa Makka Yule anaetekeleza Umrah inapendezeshwa kwake yeye aoge mara tu anapofika mji huo mtukufu, baada ya hapo aelekee masjidil-haram kulipo nyumba kongwe ya Allah, ili kutekeleza matendo yake ya umrah na ikiwa atakwenda bila ya kuoga hamna makosa

2) Hujaji anapotaka kuingia katika msikiti huo mtukufu atatanguliza mguu wa kulia na kusema:

(اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَسَلِّمْ، اللَّهُمَّ افْتَحْ لِيْ أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ).

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

“Allahumma swalli a’laa Muhammad wasallim, Allahumma iftahliy abuwaaba rahmatika”.

Maana yake: “Ewe Allah msalie na mmiminie salamu juu ya Mtume wako Muhammad, ewe Allah nakuomba nifungulie milango ya rehma zako”. Au atasema dua hii ifuatayo:

(أَعُوْذُ بِاللهِ العَظِيْمِ وَبِوَجْهِهِ الكَرِيْمِ وَسُلْطَانِهِ القَدِيْمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيْمِ)

WASIOJUA KIARABU WATASEMA
“Audhubillahil-adhwiim wabiwajhihil-kariim wasultwaanihil-Qadiim mina shaytwaani rrajiim”.

Na dua hizi ndizo za kuingia msikiti wowote mwengine kwa maana hata kwenye misikiti iliyopo kwenye mji wako pia utasoma dua hizi unapotaka kuingia msikitini.

3) Baada ya hapo ataelekea kwenye Al-qaabah tukufu ili kuanza twawaafu, ni katika sunnah kwa wanaume kuweka bega la kulia wazi katika twawaafu ya Umrah na Twawaaful – quduum peke yake.

4) Kisha ataanza kutufu mara saba, akianza katika hajarul-As -wad akiweza kulifikia hajarul-As-wad atalibusu bila ya kufanya fujo na kuleta msongamano wala kuwaudhi wasilamu wenzake kwa matusi, kupigana na kuwasukuma, yote haya hayafai kufanya wala si sawa, ikiwa hukuweza kufikia hajarul-As-wad, atanyoosha mkono na kuleta takbira na kusema.

(أَللهُ أَكْبَرُ)

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

“Allaahu akbar”

Na wakati wa kuleta hiyo takbira hatosimama ataleta na huku anatembea.

5) Ataendelea hivyo katika twawafu zote saba kila anapofika hajarul-As-wad ataleta takbira na ana uhuru wa kumtaja Allah (Subhaanahu wata’ala) kwa kila adhkaari (dhikri) kama kusoma Qur-ani katika twawafu na kuomba dua n.k na ajiepushe sana na kuudhi watu.

6) Anapofika katika nguzo ya yamaaniya (nayo ni ile nguzo kabla ya nguzo ya hajarul-As-wad) ataishika nguzo hiyo kwa mkono wa kulia ikiwa ataweza kufika hapo wala hataibusu wala kujipangusa mwili anapoishika kama wanavyofanya wengi wasiojua kuwa kufanya hivyo ni kukhalifu sunnah ya Mtume (Swallallaahu a’laihi wasallaam).

Ikiwa hatoweza kufikia nguzo hiyo basi atapita bila ya kushika kwa mkono wake pia ni katika sunnah anapofika hapo kuleta dua ifuatayo:

(رَبَّنَا آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الآخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ النَّارِ)

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

“Rabbanaa aatinaa fiyddunyaa hasanatan wafil-aakhirati hasanatan waqinaa ‘adhaaba nnaar”

7) Ataendelea hivyo katika twawaaf yake, akianza katika hajarul-as-wad akimaliza mzunguko hapo hadi mzunguko wa saba na ni sunna kwa wanaume kuharakisha kidogo katika mizunguko mitatu ya kuanzia twawaafu ya Umra na twawaaful-quduum peke yake.

8) Ahakikishe anaetufu awe katika hali ya twahara kutokana na hadathi kubwa na ndogo. Dalili ya haya ni kauli yake Mtume (Swallallaahu a'laihi wasallaam) alipomwambia (A'isha Radhwiyallahu a'nhaa)

(إِفْعَلِي مَا يَفْعَلُ الحَاجُّ غَيْرَ أَلاَّ تَطُوفِي بِالبَيْتِ حَتَّىٰ تَطْهُرِي)

(رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ١٦٥٠)، (وَمُسْلِم :١٢١١) مِن حَدِيْثِ عَائِشَة رَضِيَ اللهُ عَنْهَا

"Fanya (matendo yote) yale anayoyafanya hujaji, isipokuwa usitufu Al-Qaaba mpaka utoharike (uwe safi, usiwe na hadathi yoyote).

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu):

"Mtume amemkataza Aisha (Radhwiyallaahu a'nhaa) kutufu Al-Qaaba kwa sababu alikuwa katika ada yake ya hedhi kwa hiyo alikosa twahara (usafi) wa kumuezesha kutufu na akamwambia atatufu atakapotoharika, hii inaonesha kuwa yeyote anaetaka kutufu ni lazima awe tohara na hata Mtume (Swallallaahu Alaihi Wasallam) alikuwa anapotaka kutufu Al-Qaaba hutia udhu kama ilivyothibiti hilo katika kauli ya Aisha (Radhwiyallaahu a'nhaa) pale aliposema:

(لَمَّا أَرَادَ ﷺ أَنْ يَطُوْفَ تَوَضَّأَ) (رَوَاهُ مُسْلِم :١٢١١) مِن حَدِيْثِ عَائِشَة رَضِيَ اللهُ عَنْهَا

"Zama Mtume (Swallallaahu a'layhi wasallam) alipotaka kutufu (Al -Qaaba) alitia udhu.

Kwa iyo ewe hujaji lifahamu hili wala usighafilike nalo.

a) FAIDA: Lau mwanamme atamgusa mwanamke kwa lugha nyengine wamegusana baina ya mwanamke na mwanamme basi udhu wao hautenguki, na sio kama wanavyodhania baadhi ya watu na hii ndio kauli yenye nguvu katika kauli za wanavyuoni, ingawa ni haramu kukusudia kumgusa mwanamke ajnabia (Mwanamke unaeweza kumuoa).

b) Endapo hujaji atapata shaka (wasi wasi) ikawa hajui amezunguka mizunguko mingapi katika twawaafu basi ajenge juu ya dhana yake kubwa, kwa mfano yeye anadhania kuwa kuwa imma atakuwa amezunguka mara sita au mara tano lakini dhana yake kubwa ni mara sita na ataendelea ili kumalizia mzunguko wa saba, na ikiwa hakuna kwake dhana iliyoghilibu (kubwa) basi atajenga juu ya yakini nayo ni kuchukua idadi ndogo na kwa mfano tuliotoa atachukuwa idadi ya kuwa amezunguka mizunguko mitano na atamalizia miwili iliyobakia.

BAADHI YA MAKOSA YANAYOFANYWA NA HUJAJI KATIKA TWAWAAFU.

Kuna baadhi ya mahujaji katika jambo la kutufu kuna mambo huwa wanayafanya ambayo ni makosa kufanywa mambo hayo ni haya yafuatayo:

1. Baadhi ya watu hutufu na wakapita ndani ya hijri (ule ukuta mfupi uliopo mbele ya Al-Qaaba) wakiitakidi kusihi kwa twawaafu yao, na ukweli kuwa hijri ni katika Al-Qaaba na ni lazima upite njia yake ili uwe umetufu.

2. Kushika kila nguzo ya Al-Qaaba pengine na kuta za Al-Qaaba, wengine hushika kitambaa cha Al – Qaaba na mlango pia na wengine hushika Maqaamu Ibraahiim. Na haya yote ni uzushi usiokuwa na msingi wowote katika dini kwa wanawake zaidi hutunga mambo ya ajabu wakaambizana bila ya kuuliza ukweli wa hayo, ukakuta wengi hupata taabu na dhambi juu kwa kufanya mambo haya ya uzushi.

3. Katika makosa yanayofanywa kutangulia mmoja mbele na kupiga kelele na fujo kwa kunyanyua sauti na wengine kuitikia kwa fujo kwa sauti zao katika adh-kaari kama hizo huku ni kuwaudhi waislamu, na huwenda ikatolewa hoja kuwa tunawatamkisha hawajui ndo maana tunanyanyua sauti zetu juu ili wasikie, na tunawajibu kwa kuwambia hio sio hoja ya msingi bali kama mlikusudia kuwatamkisha ni vyema kuwafunza mwanzo kabisa na pia ikiwa mumewafunza mwanzoni lakini ikawa ni vigumu kuelewa basi ni vyema katika nyinyi viongozi wa taasisi mukachagua wale waliokuwa wanajua hii ibada mwanzo hadi mwisho, na kila mmoja mkampa mtu mmoja ili amuongoze katika ibada katika utaratibu mzuri na sio katika hali ya kufanya fujo na kelele kama zinavyosikilikana fujo hizo na kelele hizo kwa wale walio kwenye Twawaafu, na jambo hilo la kupiga kelele na kufanya fujo linaudhi waislamu sana na kuwaondoshea utulivu katika maombi yao, adh-kaari zao na kusoma kwao Qur-ani n.k. Kwa hivyo enyi mahujaji na enyi wasimamizi ambao mnasimamia mahujaji zindukeni katika hili.

4. Msongamano wa wanaume kwa wanawake katika Twawaafu katika Hajarul-aswad na katika Maqamu Ibraahiim kwa hivyo ni wajibu kujiepusha na misongamano hiyo.

BAADA YA KUMALIZA TWAWAAFU

Hujaji anapomaliza Twawaafu atafanya haya yafuatayo:

1. Kufunika bega lake la kulia.

2. Kusali rakaa mbili nyuma ya Maqaamu ibraahiim, na hii ni sunna iliotiliwa mkazo, atasoma katika rakaa ya kwanza Suratul Faatihah na suratul kaafiruuna, na rakaa ya pili atasoma suratul Faatiha na Ikhlaasw, na akisoma sura nyengine mbali na hizi baada ya suratul faatihah, hakuna tatizo. Dalili ya haya ni hadithi ya Abdallah ibn Umar (Radhiwayallahu a'nhuma) inavyosema:

(قَدِمَ النَّبِيُّ فَطَافَ بِالْبَيْتِ سَبْعًا، وَصَلَّى خَلْفَ المَقَامِ رَكَعْتَيْنِ، ثُمَّ خَرَجَ عَلَيْهِ الصَّلاَةُ وَالسَّلاَمُ إِلَى الصَّفَا) الحَدِيْثُ (رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ١٦٢٧)، (وَمُسْلِم :٢٩٩٩) مِن حَدِيْثِ عَبْدِ اللهِ بنِ عُمَرَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا.

Amefika Mtume (Swallallahu alaihi wasallaam) basi akatufu Al – Qaabah mara saba, na akasali rakaa mbili katika sehemu ya Maqaamu Ibraahim kisha akatoka na kuelekea Swafaa"

3. Anapomaliza kusali ataenda katika maji ya zamzam, atakunywa maji ya zam zam na kujimwagia kichwani, kwani hivyo ndivyo alivyofanya Mtume (Swallallahu alaihi wasallam).

4. Baada ya hapo atatoka Muutamiir (Yule anaefanya umra) na kuelekea Swafaa ili kutekeleza Sa’ayi mara saba, akikaribia Swafaa ataanza kwa kile alichoanza kukitaja Allah katika kitabu chake nayo ni Swafaa, na atakapokaribia Swafaa atasoma:

(إِنَّ الصَّفَا وَالْمَرْوَةَ مِنْ شَعَائِرِ اللهِ)

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

“inna swafaa wal-marwata min sha’aairi llahi”

5. Hapo atapanda Swafaa na kusimama juu yake ataelekea Al-Qaaba na kupiga takbira tatu, na ataomba na kukithirisha dua ikiwa amenyanyua mikono yake atasema:

(اللهُ أَكْبَرُ ، اللهُ أَكْبَرُ ، اللهُ أَكْبَرُ، لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ يُحْيِيْ وَيُمِيْتُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيئٍ قَدِيْرٌ، لاَ إِلَه إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيْكَ لَهُ، أَنْجَزَ وَعْدَهُ وَنَصَرَ عَبْدَهُ وَهَزَمَ الأَحْزَابَ وَحْدَهُ).

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

“Allahu akbar, Allahu akbar, Allahu akbar, laa ilaha illa llahu wahdahuu laa shariyka lahu, lahul-mulku walahul-hamdu yuhyii wayumiitu wahuwa a’laa kulli shay-in qadiir, laa ilaha illa llahu wahdahuu laa shariyka lahu, an-jaza wa’adahu wanaswara a’bdahu wahazamal-ahzaaba wahdahu”

6. Ataleta hii dhikri mara tatu, baina ya moja na nyengine ataomba dua, kwa hivyo dua itakuwa baina dhikri ya kwanza na ya pili akishaisoma ya tatu atashuka bila ya kuomba dua.

7. Mikono atanyanyua wakati wa dua pekee, ama wakati anapotaja hii dhikri hatoinua hii mikono.

8. Baada ya kumaliza atashuka aelekee Marwa, atatembea akiomba dua anayotaka, atajiombea nafsi yake, jamaa zake na waislamu kwa ujumla, atakapofika katika sehemu iliyo na alama (taa) za kijani hapo kwa wanaume watakimbia mbio sana, mpaka afike mwisho wa alama ile ya kijani, ataendelea kutembea tena kama alivyoanza mwanzo hadi afike Marwa.

9. Anapofika Marwa ataelekea Al-Qaaba na atayasema yale aliyoyasema akiwa Swafaa bila ya kusoma aya aliyoisoma mwanzo, na ataomba dua pia kama alivyofanya akiwa Swafaa, akimaliza atashuka ili kurudi tena swafaa, atatembea hadi atakapofika katika alama ya kijani atakimbia hadi afike mwisho wa alama ya kijani, kisha atakamilisha kutembea mpaka Swafaa.

Hivyo hivyo atakamilisha sa’ayi yake mara saba, kutoka swafaa hadi marwa ni mzunguko mmoja, kurudi kutoka Marwa hadi Swafaa ni mzunguko wa pili, ataendelea mpaka amalizie Marwa. Si vibaya akiwa amechoka ama afya yake haimruhusu kutembea masafa hayo apande kigari asukumwe. Kwa mwanamke mwenye ada yake ya mwezi pia anaweza kufanya sa’ayi.

BAADHI YA MAKOSA YANAYOFANYWA NA MAHUJAJI KATIKA SA'AYI

Miongoni mwa makosa yanayofanywa na hujaji akiwa katika sa'ayi ni haya yafuatayo:

1. Wengine wanapoleta takbira hunyanyua mikono kama wanavyonyanyua katika swala, hapa ni imma mtu afuate Sunnah ya Mtume (Swallallahu 'alayhi wasallam) ikiwa atapa nafasi ya kuifanya au awache kufanya lakini asizue jambo ambalo halikuamrishwa na sheria.

2. Wengine hukimbia kuanzia Swafaa hadi Marwa, na usawa ni kama tulivyoeleza juu.

3. Baadhi ya wanawake hukimbia kama wanaume baina ya alama za kijani, na usawa hili jambo kwa wanaume pasi na wanawake.

4. Katika makosa pia kusoma aya katika kila mzunguko na usawa ni kuisoma mwanzo pekee.

5. Katika makosa baadhi ya watu huhusisha kila mzunguko na dua yake khaaswa (maalum), na hii pia ni katika kamusi ya uzushi usio na msingi wowote.

6. Kinachopendekezwa katika sa'ayi ni kukithirisha kumtaja Allah (Subhaanahu wata'ala) ingawa hapo wananyanyua sauti zao sana na hili ni kosa kwa sababu ni kuwaudhi waislamu wenziwe.

7. Kufanya sa'ayi mara nyingi zaidi ya zile zinazotakiwa ambazo ni mbili katika Umrah kufanya sa'ayi na katika hijja

kufanya sa’ayi nyengine, sasa kuna baadhi ya watu wanafanya zaidi ya hizo, kufanya kwao huko ni uzushi.

8. Kusali rakaa mbili baada ya kumaliza sa’ayi pia ni uzushi

9. Kujiwekea dua maalum wakati wa kushuka vilima vya Swafaa na Marwa ikawa wanasoma dua hizo pia ni uzushi, hakuna dua maalum bali ni mtu aombe dua anazozitaka au adhkari au kusoma qur an lakini sio kujiwekea dua maalumu, pakitakidiwa kuwa ndivyo sahihi, kumbe ni uzushi.

BAADA YA HUJAJI KUMALIZA SA’AYI

Baada ya hujaji kumaliza sa’ayi atapunguza nywele zake au atazinyoa zote (kipara) na kuzinyoa zote ni bora, isipokuwa ukiwa wakati wa hijja umekaribia kwa maana ya kumaliza U’mra tu hakai sana anaingia kwenye hijja hapa kuzipunguza itakuwa ni bora ili kuzibakisha kwa ajili ya kujazinyoa wakati wa hijja, na dalili ya hili ni hadithi ya Jaabir bin Abdillah ambayo imetangulia kuitaja kwake katika kipengele cha aina za ibada za hijja, na ndani ya hadithi hiyo kuna maelezo haya yafuatayo:

(وَقَصَّرُوْا ثُمَّ أَقِيْمُوْا حَلَالاً).

“Na punguzeni na nywele zenu kisha kaeni hali ya kuwa mupo halali”

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu):

“Jambo la kunyoa ni bora zaidi kwa Yule atakaefanya ‘Umrah mapema na kukapatikana muda wa nywele kuota tena kwa ajili ya kuja kunyolewa katika ibada ya hijja, lakini ikiwa hujaji

amefanya U’mra wakati wa ibada ya hijja umefika, huyu lililobora kwake ni kuzipunguza nywele na sio kuzinyoa ili zibakie kwa ajili ya kujazinyoa kwa ajili ya ibada ya hijja, kwa hivyo mahujaji ni vyema kulifahamu hili ili mukaepukana nakuja kujiletea madhara ya kichwa kwani kichwa hunyolewa nywele (upara) kisha kupitishwa kiwembe au mashine huwenda likawaletea matatizo ya kichwa kwa hivyo zinduka juu ya hili ili upate wepesi wa uislamu kwani dini ya uislamu ni nyepesi.

TANBIHI: Kunyolewa au kupunguzwa ni lazima kuenezwa kichwa kizima na wala siyo baadhi ya sehemu za kichwa kama wanavyofanya baadhi ya watu na amma kwa wanawake kupunguza kiasi ya ncha ya kidole [1]

Kwa kufanya hivyo hujaji atakuwa amemaliza kutekeleza U’mrah yake inavyopaswa kutekelezwa, na hayo yote yalioharamishwa kwa ajili ya ihram yatakuwa ni halali, isipokuwa akiwa ni mwenye kufanya hijja ya Qiraan ama ifraad basi atabakia katika ihram.

FAIDA: Adhkari zote na dua zote katika Twawaaf na sa’ayi ni sunna zilizopendekezwa wala sio wajibu.

---

1. Na hili dalili yake ni kauli yake Mtume pale aliposema:
((لَيْسَ عَلَى النِّسَاءِ حَلْقٌ وَإِنَّمَا عَلَى النِّسَاءِ التَّقْصِيرُ)) رَوَاهُ أَبُو دَاوُدَ فِي سُنَنِه : ١٩٨٥)، وَصَحَّحَهُ الأَلْبَانِي فِي صَحِيْحِ أَبِي دَاوُدَ
“Hakuna ruhusa kwa mwanamke kunyoa, na hakika mwanamke ameruhusiwa kupunguza”..

NAMNA YA KUTEKELEZA HIJJA

Katika siku ya Tarwiya (tarehe nane ya dhul hijja au wengine wanaita mwezi nane) matendo ya siku hii ni kama ifuatavyo:-

- Hujaji atavaa ihram zake na kuhirimia hijja na yapendekezwa afanye katika kuhirimia hijja yake aliyoyafanya alivyohirimia umra, katika kuoga, kutia manukato na mengineyo, kisha anuie hijja na kuhirimia kwa kusema:

((لَبَّيْكَ حَجًّا))

WASIOJUA KIARABU WATASEMA
"Labbaika hajjan"

- Kisha atakithirisha talbia kwa sauti ili kudhihirisha sunna na kutafuta ujra (thawabu) kubwa mbele ya Allah, hili litaendelea mpaka atakapo tupa vijiwe Jamratul-a'qaba.

- Kisha ataelekea Mina kabla ya zawaal (dhuhri) mchana wa tarehe nane, na atasali Mina sala ya adhuhuri, laasiri, magharibi, isha na alfajiri na inapendekezwa kulala Mina na wala sio wajibu kulala Mina usiku wa kuamkia tarehe tisa (9).

Sunnah katika sala hizi atakazo Sali Mina awe ataziswali kwa wakati wake atazipunguza ingawa hatazijumuisha (kuzikusanya) isipokuwa sala ya magharibi na Alfajiri hazipunguzwi.

KUELEKEA A'RAFA

Amesema Allah (sub-haanahu wata'ala):

﴿لَيۡسَ عَلَيۡكُمۡ جُنَاحٌ أَن تَبۡتَغُواْ فَضۡلٗا مِّن رَّبِّكُمۡۚ فَإِذَآ أَفَضۡتُم مِّنۡ عَرَفَٰتٖ فَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ عِندَ ٱلۡمَشۡعَرِ ٱلۡحَرَامِۖ وَٱذۡكُرُوهُ كَمَا هَدَىٰكُمۡ وَإِن كُنتُم مِّن قَبۡلِهِۦ لَمِنَ ٱلضَّآلِّينَ ١٩٨ ثُمَّ أَفِيضُواْ مِنۡ حَيۡثُ أَفَاضَ ٱلنَّاسُ وَٱسۡتَغۡفِرُواْ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ ١٩٩﴾ [البَقَرَة: ١٩٨ - ١٩٩]

"Si vibaya kwenu kutafuta fadhila ya mola wenu mlezi na mtakapomiminika kutoka a'rafa mtajeni Allah kwenye Mash-a'ril haraam, na mkumbukeni kama alivyokuongoeni, ijapokuwa zamani mlikuwa miongoni mwa waliopotea, kisha miminikeni kutoka pale walipomiminika watu, na muombeni Allah msamaha hakika ya Allah ni mwenye kusamehe na mwenye kurehemu" (Baqarah aya ya 198-199).

Na Mtume (Swallallahu alaihi wasallam) amesema:

(الحَجُّ عَرَفَةٌ، فَمَنْ أَدْرَكَ عَرَفَةَ قَبْلَ طُلُوْعِ الفَجْرِ مِنْ لَيْلَةِ جَمْعٍ، فَقَدْ تَمَّ حَجُّهُ) الحَدِيْثُ (رَوَاهُ النَّسَائِي: ٣٠١٢)، (وَالتِّرْمِذِي: ٢٩٧٥) وَصَحَّحَهُ الأَلْبَانِيُّ

"Hijja ni a'rafa, basi yeyote atakae idiriki (kuiwahi) arafa kabla ya kuchomoza kwa alfajiri katika usiku wa mkusanyiko, basi hakika imetimia hijja yake".

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu):
“Maana ya ndani (Makusudio) ni kuwa yeyote atakaesimama a’rafa basi huyo hijja yake imekamilika, na hata yule aliechelewa akaja katika viwanja vya a’rafa na akasimama usiku kabla ya kuchomoza alfajiri ya usiku wa kulala Muzdalifa, akasimama kisha akawahi kufika Muzdalifa kabla ya kuchomoza kwa alfajiri huyu anahisabika ameiwahi a’rafa.

Ni sunnah siku ya arafa (tarehe tisa ya dhul-hijja) baada ya kusali Alfajiri Mina kufanya haya yafuatayo:

a) Ataelekea A’rafa (atakwenda) baada ya kuchomoza jua siku ya a’rafa, hii ni sunna, ikiwa ataelekea kabla ya kuchomoza kwa jua hamna makosa.

b) Ataleta talbia au takbira, na walikuwa maswahaba wakitoka Mina kuelekea A’rafa pamoja na Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) kuna wanaoleta takbira hawakukatazwa na kuna wanaoleta talbia hawakukatazwa.

Dalili ya haya ni hadithi ibn Umar inayosema:

وَعَنْ عَبْدِ اللهِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ: (غَدَوْنَا مَعَ رَسُوْلِ اللهِ ﷺ مِنْ منى إِلىٰ عَرَفَاتٍ، مِنَّا المُلَبِّي وَمِنَّا المُكَبِّرُ). الحَدِيْث (رَوَاهُ مُسْلِم : ٣٠٩٥) وَغَيره

“Na kutoka kwa Abdillah Ibn Umar (Radhwiyallahu anhuma) amesema: “Tulitoka mapema pamoja na Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) kutoka Mina kuelekea a’rafa wapo miongoni

mwetu walikuwa wakileta talbia na wapo miongoni mwetu wakileta takbira.
Pia imekuja katika hadithi ya Swahaba Anas (Radhwiyallahu a'nhu) inayosema:

وَلِحَدِيْثِ أَنَسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ وَقَدْ سُئِلَ: (كَيْفَ كُنْتُم تَصْنَعُونَ فِي هَذَا اليَوْمِ مَعَ رَسُوْلِ ﷺ فَقَالَ: مِنَّا المُهَلِّلُ فَلاَ يُنْكَرُ عَلَيْهِ وَمِنَّا المُكَبِّرُ فَلاَ يُنْكَرُ عَلَيْهِ). (رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ١٦٠٩)، (وَمُسْلِم :٣٠٩٧) وَغَيْرُهُمَا مِنْ حَدِيْثِ أَنَسِ ابْنِ مَالِكٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ

" Na kwa dalili ya Anas (Radhwiyallahu anhu) na kwa hakika aliulizwa : Vipi mulikuwa mkifanya katika siku hii pamoja na Mtume wa Allah (Swallallahu a'layhi wasallam)? Akasema: walikuwa miongoni mwetu wakileta tahlili kwa kusema :

(لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيْكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ يُحْيِي وَيُمِيْتُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيءٍ قَدِيْرٌ)

na wala walikuwa hawakatazwi, na miongoni mwao walikuwa wanaleta takbira na wala hawakatazwi".

c) Ataswali adhuhuri na laasiri kwa kuzipunguza (rakaa mbili) katika wakati wa mwanzo (yaani wakai wa mwanzo inapoingia adhuhuri), kwa adhana moja na iqama mbili, wala hamna sala ya sunna baina yake.

d) Hujaji yeyote ahakikishe anafika katika viwanja vya A'rafa na anakuwa ndani ya alama ambazo zilizowekwa kwa ajili ya kuonesha mipaka ya A'rafa, kwa sababu jambo la kusimama katika viwanja vya A'rafa ni nguzo na haitimii Hijja isipokuwa kwa nguzo hiyo.

KUSIMAMA A'RAFA

Kisimamo cha A'rafa kinaanza baada ya kutenguka jua na baada ya kuswaliwa swala ya adhuhuri na laasiri kwa kuzikusanya pamoja kama tulivyokwisha tangulia kueleza hili, na muda wa mwisho wa kumaliza kusimama A'rafa ni mpaka Alfajiri ya usiku wa siku ya kuchinja (mwezi kumi dhul-hijja) huo ndio muda wa mwisho wa kisimamo cha A'rafa, yeyote atakaesimama nje ya wakati huo atakuwa amekosa kisimamo cha A'rafa.

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu):

"Hapa inaelezwa kuanza muda wa mwanzo wa A'rafa na muda wa mwisho ikiwa mtu atachelewa kufika katika viwanja vya A'rafa mpaka muda gani wa mwisho ili yeye akifika awezekuhesabika ameipata A'rafa? Ndo pamesemwa mpaka alfajiri ya usiku wa kuamkia siku ya kuchinja na haina maana ya kua mtu atakaekua amesimama A'rafa kuwa asiondoke mpaka alfajiri, hii siyo maana yake, bali maana ni kuoneshwa wakati wa mwanzo na wakati wa mwisho kama vile katika nyakati za swala, kwani kila swala ya faradhi ina wakati wake wa mwanzo

na kuingia kwake na wakati wake wa mwisho wa kutoka kwake, na vile vile katika kusimama A'rafa ni kama hivyo"

Baada ya kusali Adhuhuri na Laasiri atayafanya haya yafuatayo:

1. Atasimama katika mawe yaliyochini ya Jabal-rahma ikiwa siyo takliif kwake, la si hivyo Mtume (Swallahu Alaihi wasallaam) amesema: "Nimesimama hapa na A'rafa yote ni sehemu ya kusimama.

2. Yapendekezwa kuelekea qibla wakati huo huo ukiwa umeelekea Jabal-rahma ikiwa itawezekana, isipowezekana basi ataelekea qibla hata ikibidi jabal-rahma kuwa nyuma yake.

3. Atanyanyua mikono yake na kuomba kwa unyenyekevu na akileta talbiya pia na kusoma Qur-ani ni vizuri.

4. Na inapendekezwa zaidi kukithirisha tahlili kwani ni bora wa kilichosemwa siku ya A'rafa tahlili yenyewe ni kama ifuatayo.

(لاَ إِلَهَ إِلاَّ اللهُ وَحْدَهُ لاَشَرِيْكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ يُحْيِي وَيُمِيْتُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيءٍ قَدِيْرٌ).

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

"Laa ilaha illa llahu wahdahuu laa shariyka lahu, lahul-mulku walahul-hamdu yuhyii wayumiitu wahuwa 'alaa kulli shay-in qadiir"

5. Ni sunna kwa aliyesimama A'rafa, asifunge siku hiyo kwa kumfuata Mtume kwani Mtume (Swallahu a'layhi wasallam)

hakufunga siku hiyo aliposimama A’rafa na dalili ya hayo ni hadithi hii ifatuatayo:

(أَنَّ نَاسًا تَمَارَوْا عِنْدَهَا (اخْتَلَفُوا عِنْدَهَا) يَوْمَ عَرَفَةَ فِي صَوْمِ النَّبِيِّ فَقَالَ بَعْضُهُم هُوَ صَائِمٌ وَقَالَ بَعْضُهُم لَيْسَ بِصَائِمٍ، فَأَرْسَلَتْ إِلَيْهِ بِقَدَحِ لَبَنٍ وَهُوَ وَاقِفٌ عَلَى بَعِيرِهِ فَشَرِبَــهُ). (رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ١٩٨٨)، (وَمُسْلِم :١١٢٣) مِنْ حَدِيْثِ أُمِّ الفَضْلِ رَضِيَ اللهُ عَنْهَا.

“Hakika watu walizozana na kutofautiana mbele yake (Ummul – fadhwli) siku ya A’rafa kuhusu kufunga kwa Mtume (Swallahu a’layhi wasallam) wakasema baadhi yao, kua Mtume amefunga na wakasema baadhi yao hajafunga, basi akapeleka (akampelekea) glasi ya maziwa na hali ya kuwa Mtume amesimama juu ya ba’iru (ngamia) Mtume akanywa (maziwa hayo)”

6. Ataendelea katika hali hii, kumtaja allah, kuleta talbiya, kuomba dua akitarajia kwa mola wake amjaalie katika wale atakao waachilia huru na moto.

7. Litakapotua jua, ataondoka na kuelekea Muzdalifa kwa utulivu na unyenyekevu na kukithirisha talbiya na pasi na kumuudhi mtu.

8. Wala haijuzu kuondoka A’rafa kabla ya kutua kwa jua, kwa sababu Mtume alisimama A’rafa hadi lilipotua jua.

BAADHI YA MAKOSA YANAYOFANYWA NA BAADHI YA WATU KATIKA A'RAFA

Miongoni mwa makosa yanayofanywa na watu wakiwa A'rafa ni haya yafuatayo:-

1. Wengine hushukia nje ya mpaka wa A'rafa na hubaki sehemu hizo mpaka kutua kwa jua, na hili ni kosa kubwa mno, kwani anaefanya hivyo hana hijja.

2. Wengine huondoka A'rafa kabla ya kutua kwa jua, na hili ni kinyume na sunna ya Mtume (Swallallaahu alaihi wasallam) kwani yeye alisimama hadi lilipotua jua, na pia kwa sababu kuondoka kabla ya kutua kwa jua ni katika vitendo vya jahiliya (vitendo vilivyokuwa vikifanywa zama za kijinga kabla ya kuja Mtume na kabla ya utume).

3. Kujikalifisha baadhi ya watu kupanda juu ya Jabal-rahma, na kujikalifisha huku hakuna dalili bali ni uzushi katika dini, kama walivyotanabahisha wana chuoni.

4. Kuelekea Jabal-rahma wakati wa dua na kutoelekea Qibla, na hii ni kinyume na sunna.

5. Kuswali sunna baina ya swala ya Adhuhuri na Laasiri, kwani Mtume hakufanya hivyo.

6. Ni katika makosa vile vile kutanguliza swala ya adhuhuri na laasiri kabla ya khutba, wengi wa watu huswali kwanza kisha ndo hutoa khutba, kufanya kwao hivi ni makosa na lililokuwa sahihi ni khutba inatangulia kisha ndo swala.

7. Kunyamaza kimya na kutojishughulisha na dua pamoja na adhkari katika viwanja vya arafa (yaani wakati mtu yupo A'rafa).

KULALA MUZDALIFA

Baada ya kutua na kuzama kwa jua katika siku ya A'rafa hujaji ataelekea Muzdalifa kwa upole na utulive na kutowaudhi watu katika kuondoka kwake. Na akifika Muzdalifa atatakikana ahakikishe kuwa yumo ndani ya maeneo ya Muzdalifa kwa sababu akiwa nje ya maeneo ya muzdalifa kulala kwake kutakuwa na mapungufu.

Yale ambayo anatakikana ayafanye hujaji akiwa Muzdalifa ni haya yafuatayo:

1) Anapofika Muzdalifa wakati wa swala ya magharibi au ishaa, ataswali swala hizo mbili kwa kuzijumuisha na kuzipunguza (Swala ya magharibi itabaki tatu) kwa adhana moja na iqama mbili, wala hatoswali baina yake swala ya sunna, akiogopea kufika muzdalifa kabla ya nusu ya usiku ataswali swala hizo njiani kwa kuchelea kupita nusu ya usiku kabla ya kuswali swala hizo.

2) Na atalala Muzdalifa, na kulala kwake Muzdalifa ni wajibu na ni vyema (inapendezeshwa) baada ya kumaliza kuswali swala ya Magharibi na isha, alale na wala asijishughulishe na kuokota vijiwe, kwani Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) aliswali magharibi na isha kisha akalala wala hakuamrisha kuokota

vijiwe isipokuwa baada ya kuondoka Muzdalifa na inajuzu kuokota vijiwe hata Mina.

3) Wala sio sunna kuosha vijiwe hivyo.

4) Yajuzu kwa wanawake kuondoka Muzdalifa baada ya nusu ya usiku, kadhalika madhaifu kama watu wazima na watoto, kadhalika anayekuwa pamoja na wao katika wenye nguvu zao.

Mtume (Swallahu alaihi wasallaam) kuwa amewaruhusu wanawake, watoto na mfano wao kuondoka kwao Muzdalifa baada ya nusu ya usiku kama ilivyokuja katika hadithi ya Abdillah bin Omar, na hadithi ya Abillah bin Abbas na hadithi ya Asmaa bint Abuubakar na hadithi ya A'isha (Radhwiyallahu a'nhum) Hadithi zote hizo zipo katika sahhi Bukhari na Sahihi Muslim.

5) Sunna ni kulala Muzdalifa usiku huo mpaka alfajiri, na waswali alfajiri Muzdalifa.

6) Baada ya kuswali alfajiri Muzdalifa inapendekezwa kusimama katika Mash-aril haram (nalo ni jabal liliyoko Muzdalifa) au kusimama sehemu yoyote ya Muzdalifa ataelekea qibla na kukithirisha kumtaja Allah na kuomba dua kwa wingi.

7) Baada ya hapo ataondoka kabla ya kuchomoza kwa jua na njiani ataokota vijiwe saba, ukubwa wa tembe ya maharagwe, ili kutupa vijiwe hivyo katika Jamaratul - a'qaba na vijiwe vilivyobakia atachukulia Mina.

Ataelekea Mina kwa utulivu na unyenyekevu huku akileta talbiya:

(لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ لاَشَرِيْكَ لَكَ لَبَّيْكَ، إِنَّ الحَمْدَ وَالنِّعْمَةَ لَكَ وَالمُلْكُ لاَشَرِيْكَ لَكَ).

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

“Labbaika llaahumma labbaika, labbaika laa shariika laka labbaika, innal-hamda wanneamata laka wal-mulku laa shariika laka”

MATENDO YA SIKU YA IDDI (TAREHE KUMI DHUL-HIJJA)

Matendo ya hujaji katika siku hii ya iddi ya tarehe kumi dhul-hijja ni manne (4), na ni bora afuatilize katika utaratibu ufuatao:-

1. Kutupa vijiwe katika Jamaratul-A’qaba.
2. Kuchinja.
3. Kunyoa au kupunguza nywele.
4. Kutufu nyumba ya Allah na kufanya sa’ayi kwa mutamattui, kadhalika aliyefanya hajji ya Qiraan au Ifraad ikiwa hakufanya sa’ayi katika twawaaful-quduum.

Na hata asipofuatilia utartibu huu, hijja yake ni sahihi na hana kosa lolote.

Inaingia katika hayo pia kutanguliza Sa’ayi kabla ya twawaafu kwani imethibiti kuwa Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) aliulizwa juu ya yule aliyetanguliza sa’ayi kabla ya twawaafu

akajibu “Haina neno” kama ilivyokuja lafdhi (tamko) ya hadithi ifuatayo:

(أَنَّ النَّبِيَّ ﷺ سُئِلَ عَمَّنْ قَدَّمَ السَّعْيَ عَلَى الطَّوَافِ فَقَالَ لاَ حَرَجَ). مِنْ حَدِيْثِ أُسَامَةَ ابْنِ شَرِيْكٍ

Hadithi hii na nyenginezo zenye maana hii lakini kwa matamko mengine ni hadithi sahihi baadhi yake zimo katika sahihi bukhari (1735) na (1722) na nyengine zimo katika sahihil-muslim (3156) na (3163) na vitabu nyenginezo.

Na kutapatikana kuhalalika kikamilifu kwa mambo matatu (kutupa vijiwe, kunyoa au kupunguza, twaaful-ifaadha pamoja na sa’ayi) akifanya mambo haya matatu, ni halali kwake kila kilichoharamishwa wakati yupo kwenye ihram, hata kumkaribia mke wake pia. Ama akifanya mawili katika haya, basi atahalalika kila kitu alichokatazwa wakati wa ihram ila mke wake hataruhusiwa kumkaribia mpaka afanye yote matatu.

KUTUPA VIJWE JAMRATUL – AQABA KUBWA SIKU YA IDDI

Katika siku ya iddi (siku ya kumi na kuchinja-Dhulhijja) hatatupa vijiwe isipokuwa katika Jamratul-a’qaba kubwa kwa namna ifuatavyo.

1) Anapofika Mina baada ya kutoka Muzdalifa ataelekea kwenye Jamratul-A’qaba kubwa atakapofika atakata talbiya ili kujishughulisha na kutupa vijiwe.

2) Kisha atatupa vijiwe saba kwa kufuatana (kimoja baada ya

chengine) na lau kama atatupa yote saba kwa pamoja basi itahesabika ni kama aliyetupa kijiwe kimoja kwa hivyo ni lazima atupe kimoja baada ya chengine.

3) Kila anapotupa kijiwe atapiga takbira kwa kusema “Allahu Akbar”

4) Ni lazima ahakikishe kila kijiwe kimeingia ndani ya shimo liliyoko katika jamratul-a’qaba kwani la muhimu ni kijiwe kuingia ndani ya shimo wala sio kupiga ukuta.

5) Wala sio sunna kusimama na kuomba dua baada ya kutupa vijiwe katika siku hii.

6) Wala asitumie vijiwe vilivyotumika ingawa akitumia itamtosheleza ila ni bora ajiepushe nalo hili la kutumia vijiwe vilivyokuwisha kutumika.

7) Na wakati wa kutupa vijiwe katika Jamratul-a’qaba kubwa ni kuanzia nusu ya usiku wa kuamkia tarehe kumi (siku ya iddi), na pia aweza kutupa vijiwe baada ya adhuhuri mchana wa siku ya iddi, hata ikifika usiku, kwa sababu hakuna dalili inayokataza kutupa vijiwe vya siku hiyo katika usiku wa kuamkia tarehe kumi na moja.

8) Ama kutupa vijiwe kabla ya Adhuhuri katika masiku ya Tashriq (tarehe 11,12, na 13 ya dhulhijja) **HAIJUZU WALA HAITOSHELEZI,** kwa sababu hakika Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) alitupa vijiwe katika masiku ya Tashriq baada ya adhuhuri (zawali) na pia masahaba wake, na lau kama kungalikuwa na ruhusa angalibainisha Mtume ruhusa hiyo kwa

sababu kusubiri mpaka wakati wa zawali kuna uzito pamoja na uzito huo hakufanya yeye wala hakuwapa idhini walio madhaifu na mfano wao kutangulia kutupa vijiwe siku hizo, kama Alivyowapa ruhusa kuondoka Muzdalifa mapema, na hii ni dalili ya wazi ya kuwa **HAIJUZU WALA HAITOSHELEZI KUTUPA VIJIWE KABLA YA ZAWALI.**

Na hii ndiyo kauli ya Imam malik, Abuu hanifa, Shafii na Ahmad. Hawa ni maimamu wanne ndiyo msimamo wao ambao hawa madhehebu yao ni maarufu na yameenea zaidi kila kona ya dunia na ndiyo kauli inayoambatana na sunna ya Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam).

9) Yajuzu kumwakilisha mtu mwengine atupe vijiwe kwa niaba ya yule asiekuwa na uwezo wa kutupa vijiwe mwenyewe, kama mgonjwa au mtu mzima au kipofu ambao kwao wao ni uzito kwenda kutupa vijiwe wenyewe, watamtuma mtu atakaewakilisha katika jambo hilo, ama mwenye uwezo wa kufanya hivyo kwa nafsi yake, basi haijuzu kuwakilisha mtu amtupie na lau kama atawakilisha mtu basi haitomtosheleza.

10) Na mtu aliyewakilshwa katika kumtupia vijiwe mtu mwengine, mwanzo aanze na kujitupia vijiwe vyake, kabla ya kumtupia yule anayemuwakilisha, wala haijuzu kwa asiyekuwa katika matendo ya hijja kumwakilisha anaefanya hijja.

KUCHINJA SIKU YA IDDI

Baada ya kutupa vijiwe siku ya kumi basi atafanya haya yafuatayo:

1. Hajji (Hujaji) atakuja shemu ya kuchinja iliyoko Mina atachinja wanyama wake, hivi ndivyo ilivyo sunna, kutupa vijiwe kisha kuchija ingawa si lazima. Dalili ya hili jambo la kuchinja katika sehemu za Mina ni kauli yake Mtume (sala na salamu zie juu yake) pale aliposema:

(قَدْ نَحَرْتُ هَهُنَا، وَمِنَى كُلُّهَا مَنْحَرٌ، وَكُلُ فِجَاجِ مَكَّةَ طَرِيْقٌ وَمَنْحَرٌ فَانْحَرُوا فِي رِحَالِكُمْ) (أَخْرَجَهُ مُسْلِم : ١٢١٨)، (وَأَبُو دَوُدَ :١٩٣٧) (وَالنَّسَائِيُّ :٣٠١٥)، (وَأَحْمَدُ :١٤٤٩٨).

“ Hakika mimi (Mtume wenu) nimechinja hapa, na mina yote ni sehemu ya kuchinja, na kila kichochoro cha Makka (njia kubwa za Makka) ni njia zinazohusiana kupita na ni sehemu za kuchinja, basi chinjeni majumbani mwenu”

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu): hii hadhithi imekuja weka wasaa mkubwa kuhusu eneo la kuchinja hata eneo la nyumba za makkah, mtu anaruhusika kuchinja ila serikali ya Saudia kwa kuwafanyia wepesi mahujaji jambo hili wamechukua dhamana wao kwa kuteua baadhi ya viongozi wa taasisi za mahujaji wakishirikiana nao kwa ajili ya kulisimamia wao wenyewe ili kumfanyia wepesi hujaji, na kuepusha

misongamano ambayo mara nyingi hupelekea kufa kwa baadhi ya mahujaji, na hivo vichinjwa huchinjwa ndani ya mipaka ya haram na sio nje yake.

FAIDA (a): Sunna katika ibada ya kuchinja ni mtu achinje kwa mkono wake ikiwa inawepesika kufanya hivyo, na ikiwa ni ngumu kuchinja yeye mwenyewe basi atawakilisha mtu wa kumchinjia kama walivyoeleza wanachuoni kwa kauli yao hii ifuatayo:

[السُّنَّةُ أَنْ يَذْبَحَ أَوْ يَنْحَرَ بِيَدِهِ، إِنْ تَيَسَّرَ لَهُ، وَإِلاَّ أَنَابَ عَنْهُ غَيْرُهُ]

“Na sunna ni kuchinja (kumwaga damu) mnyama kwa mkono wake hujaji) ikiwepesika kufanya hivyo na ikiwa haijawepesika atamkalia niaba mwengine kumchinjia”

b) Ni sunna wakati wa kuchinja yule mnyama kumuelekeza kibla, na hii ni kwa hujaji na asiyekuwa hujaji pia ni sunna kufanya hivyo.

2. Na inajuzu kwa watu saba kushirikiana katika kuchinja ngamia mmoja au ng’ombe mmoja, na hiyo itawatosheleza.

3. Na asiyekuwa na uwezo wa kuchinja basi atafunga siku tatu (3) katika hijja na saba (7) atakaporudi kwao.

4. Ana uhuru katika kufunga kwake swaumu hiyo siku tatu akitaka atafunga kabla ya siku ya iddi na akitaka atafunga masiku ya tashriq matatu (11,12 na 13) au lugha iliyobora zaidi ni tarehe (11,12 na 13) katika masiku ya kuanika nyama.

5. Na ni bora zaidi ikiwa atafunga siku hizo iwe ni kabla ya siku ya iddi, na pia afunge kabla ya siku ya A'rafa, kwa sababu Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) alisimama A'rafa akiwa hakufunga na alikataza mahujaji kufunga siku hiyo ya A'rafa hujaji akiwa hajafunga inakuwa ni uchangamfu kwake zaidi kumtaja Allah na kumuomba dua.

6. Na wakati wa kuchinja ni siku nne siku ya iddi na masiku ya tashriq (11, 12 na 13).

KUPUNGUZA NYWELE NA KUNYOA (KIPARA) SIKU YA IDDI

Katika siku ya mwezi kumi (tarehemu 10 ya dhul-hijja) katika matendo au miongoni mwa matendo ya kufanywa siku hiyo ni kunyoa ili kulifahamu vizuri hili zingatia vipengele vifuatavyo:

1) Ni sunna kufanyika jambo la kunyoa iwe baada ya kutupa vijiwe na kuchinja, ingawa akitanguliza mwanzo kunyoa itajuzu.

2) Atanyoa kichwa chake chote (kipara) au atapunguza kichwa chake chote wala haitoshelezi kupunguza baadhi ya sehemu za kichwa na kunyoa (kipara) ni bora zaidi.

TANBIHI: Kuna baadhi ya watu wanapomaliza hijja huwa wanafanya u'mra na ikifika wakati wa kunyoa hunyoa baadhi ya sehemu za kichwa na kuacha sehemu nyengine na kurudi tena, na kuifanya u'mra nyengine ili zile nywele zilizobakia sehemu ya kichwa azinyoe kwa u'mra ya pili, kufanya kwao huku ni makosa na kunyoa kwao huku hakuwatoshelezi, bali

kinachotakikana ni kupunguza kichwa kizima au kunyoa kichwa chote na siyo baadhi. Mara nyingi watu wa aina hii wanakuwa wamechukua pesa za watu ili kuwafanyia u'mra watu hao waliyotoa pesa hizo, kwa hiyo pesa hizo huchukuwa wao na kuwafanyia u'mra katika namna hiyo tulokwisha ieleza ya kuwa wakifika wakati wa kunyoa hunyoa baadhi ya sehemu ya kichwa tu na baki ya sehemu ya kichwa kwa ajili ya 'umra ya mtu mwengine.

Na wengine wanakuwa hawajachukua pesa ya mtu bali mtu ameamua kuwafanyia u'mra watu wake, ima wazazi wake au walimu wake na mfano wa hao, kwa hiyo huwa wananyoa baadhi ya sehemu ya kichwa na kubakisha sehemu nyengine kwa ajili ya u'mra nyeingine, bali wengine hata katika ibada ya hijja yenyewe hutoa baadhi ya nywele kwa maana sehemu ya kichwa tu kama vile kisogoni (kichogoni) au pembeni au katikati na zilizobakia ni kwa ajili ya umra alizokusudia kufanya. Na hapa napenda kuweka kauli za maulamaa juu ya jambo hili ili wepesi upatikane kwa kila yule mwenye kutaka wepesi wa kisheria na sio wa kiakili yake.

a) Kauli ya mwanzo ya Sheikh Ibnu Baazi:

[قَالَ العَلاَّمَةُ ابْنُ بَازٍ رَحِمَهُ اللَّهُ فِي (التَّحْقِيْقِ وَالإِيْضَاحِ: ص٤٠): وَلاَ يَكْفِي تَقْصِيْرُ بَعْضِ الرَّأسِ بَلْ لاَ بُدَّ مِنْ تَقْصِيْرِهِ كُلِّهِ كَالْحَلْقِ]

"Na wala haitoshelezi kupunguza baadhi ya sehemu ya kichwa bali hapana budi kupunguza nywele za kichwa kizima kama katika kunyoa ilivyokuwa kunyolewa kichwa kizima"

b) Kauli ya pili ya Sheikh Albaniy:

[قَالَ العَلاَّمَةُ الأَلْبَانِي رَحِمَهُ اللهُ فِي (مَنَاسِكِ الحَجِّ وَالعُمْرَةِ : ص٣٥): ثُمَّ يَحْلِقُ رَأسَهُ كُلَّهُ أَوْ يُقَصِّرَهُ].

“Kisha atanyoa kichwa chake chote (kizima) au ataupunguza chote (kizima).

c) Kauli ya tatu ya Sheikh Abdul-Muhsin:

[قَالَ العَلاَّمَةُ عَبْدُ المُحْسِنِ العَبَّـادِ رَحِمَهُ اللهُ فِي (تَبْصِيرِ النَّاسِكِ بِأَحْكَامِ المَنَاسِكِ): فَلاَ يَكْفِي أَنْ يُقَصِّرَ بَعْضَ شَعْرِ الرَّأسِ وَيَتْرُكَ بَعْضَهُ كَمَا أَنَّهُ لاَ يَكْفِي أَنْ يَحْلِقَ بَعْضَ الرَّأسِ وَيَتْرُكَ بَعْضَهُ].

“Basi haitoshelezi (haifai) kupunguza baadhi ya sehemu ya kichwa na kuacha baadhi ya sehemu yake, kama ilivyokuwa haitosehelezi kunyoa baadhi ya sehemu ya kichwa na kuacha baadhi yake”.

Nimesema hapa (Abuu Muhammad): Kauli za maulamaa zipo nyingi sana sitoziweka zote kwa kuchelea kurefuka kwa kitabu na nitafupilizika na kuali tatu hizo ambazo nimeshaziweka na kuzitolea maana zake. Huenda mtu akasema “Lakini mimi napuguza au kunyoa baadhi na kubakisha baadhi ili nipate kutekeleza u’mra nilizokusudia na wala sikusudii kunyoa au kupunguza baadhi kisha nikae nazo hivyo hivyo kama wafanyavyo vijana hunyoa baadhi na kubakisha baadhi, staili ambayo wanaita **“PANKI”**

Jawabu: Hijja ni ibada aliyoifundisha Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) na u'mra hali kadhaalika, sasa haya mnayoyafanya nyinyi sio aliyoyafundisha Mtume wetu kipenzi, kwa hiyo ni lazima myawache hayo mnayoyafanya na mufuate mwenendo wa Mtume katika ibada ya u'mra, ibada ya hijja na ibada zake zote na hazitokuwa ibada za mtu ni nzuri mpaka pale atakapomfuata Mtume katika ibada zake zote na bila ya kuzua jambo linalokwenda kinyume na mwenendo wake.

Kwa hiyo haya wanayoyafanya watu baada ya kumaliza ibada ya hijja na kuanza kufanya u'mra zao kwa kunyoa na kupunguza baadhi ya sehemu na kubakisha sehemu ya kichwa ni makosa na Haifai kufanya hivyo basi zinduka ewe Muislamu juu ya kosa hili [1]

3. Na ikiwa mtu alipunguza baadhi ya sehemu za kichwa pasi na kujua hukmu yake basi itamtosheleza.
4) Na hii ni sunna aanze kinyozi kunyoa upande wa kulia wa kichwa, kama alivyoeleza Mtume katika hadithi iliyopokelewa na swahaba wake Anas bin Malik (angalia sahihi-muslim na kitabu al-ir-waail-ghaliil, 964).

---

1. Nimesema hapa Abuu Muhammad Hasnuu: Jambo la kufanya 'umra kwa kutumia kituo cha TANIIMU au kwa jina jengine MASJID-AISHA baada ya kumaliza hijja ni jambo ambalo lina ikhtilafu kufaa kwake.

5) Ama kwa mwanamke atapunguza kwa kadri ya ncha ya kidole baada ya kukusanya nywele zake pamoja kama tulivyokwisha kueleza katika matendo ya umra, na tukasema mwanamke hakuna kwake yeye hukumu ya kunyoa bali ni kupunguza kiasi cha ncha ya kidole kwa dalili ya kauli ya Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) na makubaliano ya maulamaa wote.

(لَيْسَ عَلَى النِّسَاءِ الحَلْقُ، إِنَّمَا عَلَى النِّسَاءِ التَّقْصِيْرُ).

Amesema Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam): "Hakuna juu ya mwanamke jambo la kunyoa bali kilichokuwa (lililokuwepo) juu ya wanawake ni jambo la kupunguza tu" hadithi maelezo yake yamekwisha tangulia.

[قَالَ ابْنُ المُنْذِرِ رَحِمَهُ اللَّهُ فِي (الإِجْمَاعِ : ص٦٦): وَأَجْمَعُوا أَنْ لَيْسَ عَلَى النِّسَاءِ حَلْقٌ].

"Na wamekubaliana (wanachuoni) ya kwamba hakuna kwa wanawake jambo la kunyoa.

TWAWAAFUL-IFAADHA

Hii ni twawaafu (Kutufu Al-qaabah) ambayo wakati wake ni kuanzia baada ya nusu ya usiku wa kuamkia iddi, baada ya mahujaji kuondoka muzdalifa.

1. Twawaafu hii ni nguzo katika nguzo za hijja.

2. Haitosihi twawaafu hii endapo itatekelezwa kabla ya hujaji kusimama A'rafa.

3. Na ni sunna kwa twawaafu hii iwe baada ya kutupa vijiwe, kuchinja na kunyoa nywele ingawa yajuzu kuitanguliza.

NAMNA YA KUITEKELEZA TWAWAAFU HII

Namna ya kuitekeleza twawaafu hii ni kama ifuatavyo:

1. Anapohalalika kwa kwanza, nako kuhalalika huko hupatikana kwa mtu kufanya haya yafuatayo:

a) Kutupa vijiwe katika nguzo kubwa ndani ya siku ya kumi ya mwezi wa dhul-hijja (siku ya kuchinja).

b) Kunyoa au kupunguza nywele.

Kwa kufanya haya mawili hujaji atahesabika amehalalika kwa, kwanza ameruhusika kwa kujitia manukato na baada ya kujitia manukato atakwenda msikiti wa Makkah kwa ajili ya tawaafu.

2. Atatufu mara saba, kwa namna tulivyokwisha eleza mwanzo, isipokuwa hatowacha bega lake nje au kuacha wazi wala hatotufu upesi katika mizunguko ya mwanzo mitatu kama alivyofanya katika Twawaaful-quduum.

3. Na ni katika sunnah kusali rakaa mbili baada ya twawaafu kama tulivyoeleza mwanzo

4. Baada ya hapo kwa mwenye kufanya hijja ya tamattui atafanya sa’ayi baina ya swafwaa na mar-wa kwa namna ilivyotangulia maelezo yake.

5. Kufikia hapa lazima ijulikane na ifahamike kuwa mwenye kufanya hijja ya tamattui atafanya sa’ayi mara mbili, ya kwanza

anapofanya u’mrah, na ya pili kwa ajili ya hijja yake wala haimtoshelezi sai moja.

6. Baada ya twawaafu hii atakuwa amehalalika kikamilifu, na ni halali kwa kila kilichoharamishwa na ihram hata jambo la kumkaribia mkewe na kufanya tendo la jimai na hii ndio inayoitwa kuhalalika kwa pili.

7. Baada ya hapo atakwenda kwenye maji ya zam zam na atakunywa maji ya zam zam na kujimwagia kichwani.

8. Kwa mwanamke aliepata ada ya mwezi kabla ya kutufu twawaafu hii atasubiri pamoja na mahrimu wake mpaka atoharike ikiwa hakumakinika kwa kuifanya twawaafu hiyo kwa kuhitajika kurudi nchi yake kabla ya kutwaharika atasafiri kwenda kwao, na baadae atarudi atakapotoharika ili kuja kuitekeleza twawaafu hii, na ama ikiwa ni mkaazi wa nchi za mbali hapo itajuzu kwake kuvaa kitakachomhifadhi damu isimtoke na kudondokea chini kisha atatufu kwa nia ya hijja na itamtosheleza, na hii ni kauli ya baadhi ya wanachuoni japo kuwa zipo kauli nyengine katika mas-ala haya.

9. Baada ya kumaliza twawaafu hii na kusali rakaa mbili katika Maqaamu-ibraahim, na baada ya kunywa maji ya zam zam na baada ya kufanya sa’ayi hujaji atalazimika arudi zake Mina kwa ajili ya kutekeleza yanayowajibisha sheria kuyafanya huko Mina kama tutakavyoeleza katika haya yanayofuata.

KULALA MINA

Jambo la kulala mina kwa mahujaji ni katika mambo ya wajibu katika ibada yao ya hijja. Na hujaji baada ya kumaliza

twawaaful-ifaadha na sa’ayi, atarejea Mina na atabaki huko Mina siku hiyo ya iddi na masiku ya tashriq nayo ni siku tatu mchana na usiku na mpangilio wake ni huu ufuatao:

A. Siku ya kumi na moja dhul-hijja 11

B. Siku ya kumi na mbili dhul-hijja 12

C. Siku ya kumi na tatu dhul-hijja 13

UFAFANUZI NA UBAINIFU WA KULALA MINA

Katika ibada hii mahujaji kuwepo mina kwa siku hizi ambazo sheria imewataka wakuwepo katika viwanja hivyo ni vyema kuweka ubainifu juu ya kuwepo kwao maeneo hayo pamoja na kufafanua kama ifuatavyo:

1. Kinachozingatiwa katika jambo hili la kulala Mina ni kupitisha sehemu kubwa ya usiku katika maeneo hayo, kwa sababu sheria haikuweka mipaka katika muda wa kulala Mina, kwa mfano usiku una masaa kumi sasa hujaji akakaa masaa sita au saba yatamtosheleza na kuhesabika kuwa amelala Mina na kuwa ametekeleza uwajibu wa yeye kuwepo Mina.

2. Hakuna kosa kwa yule aliye na uzito akiwa atakaa mchana wake Makka na usiku arudi Mina ni bora kwake kukaa Mina usiku na mchana

3. Yajuzu kwa hujaji kuzuru na kuitembelea Al-qaaba na kutufu katika kila usiku wa Mina kwa sababu Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) alifanya hivyo.

4. Na ni wajibu kwa hujaji kusali sala zake tano kwa jamaa na lililokuwa bora zaidi ni kusali katika msikiti wa Khaifu ikiwepesika kwa hujaji huyo wakati akiwa yupo Mina na ikiwa

itakuwa ni vigumu basi atasali katika mahema yao. Dalili la pendekezo la kusali katika msikiti wa Khaifu ambao upo Mina ni hii ifuatayo:

وَعَن عَبْدِ االله ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: (قَالَ رَسُولُ اللهِ ﷺ: صَلَّى فِي مَسْجِدِ الخَيْفِ سَبْعُوْنَ نَبِيـًّا) (أَخْرَجَهُ الطَّبْرَانِيُّ ٤٥٣/١١) وَحَسَّنَهُ الأَلْبَانِيُّ فِي (مَنَاسِكِ الحَجِّ وَالعُمْرَةِ : ٣٩) و (تَحْذِيْرِ السَّاجِدِ : ٩٧).

“Kutoka kwa Abdillahi ibnu Abbas (Radhwiyallahu a’nhu) amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallahu a’layhi wasallam) wamesali katika mskiti wa khaifu (Masjidil-Khaifu) Mitume sabini”

Nimesema hapa (Abuu Muhammad hasnuu) “Masjidil-Khaifu upo sehemu za Mina na karibu na nguzo ya mwanzo kurembewa mawe, na katika maulamaa waliokwenda na kauli ya kusema ni bora kusali hapo ni shekhe Albaniy (Rahimahullahu) lakini ikiwepesika na ikiwa haijawepesika ni vyema mtu kuswali katika mahema kuliko mtu kujitia katika shida, zahma, kujichosha na kujiumiza jambo ambalo hupelekea mara nyingi kuwaudhi na wengine na kuwaletea madhara vile vile, lililokuwa bora ikiwa hujaji ataona kuwa kuna zahma na msongamano au kipande ni kikubwa maana masafa alipo yeye katika hema lake na ulipo msikiti ni mbali kwa namna ambayo itampelekea kuchoka sana au hata kukosa jamaa basi lililobora ni kusali jamaa katika mahema.

5. Na ni juu ya kila aliye katika ibada ya hijja kukithirishakumtaja Allah katika masiku haya machache. Na dalili ya haya ni kauli ya Allah (Subhaanahu wata'ala) pale aliposema:-

﴿ وَٱذۡكُرُواْ ٱللَّهَ فِيٓ أَيَّامٖ مَّعۡدُودَٰتٖ ﴾ [البَقَرَة : ٢٠٣]

"Na mtajeni Allah katika siku zinazohisabiwa"

قَالَ ابْنُ عَبَّاسٍ: (الأَيَّامُ المَعْدُودَاتُ أَيَّامُ التَّشْرِيْقِ وَالأَيَّامُ المَعْلُومَاتُ: أَيَّامُ العَشْرِ).

Amesema Ibnu Abbas (Radhwiyallahu a'nhu)

"Siku zinazohisabiwa ni zile siku za Tashriq (siku za kuanika nyama mwezi 11, 12 na 13) na siku maalum ni zile siku za kumi la mwanzo la mwezi wa dhul-hijja"

KUTUPA VIJIWE KATIKA VIKUTA AU VIGUZO KATIKA MASIKU YA TASHRIQ (MWEZI AU TAREHE YA KIISLAM 11,12 NA 13)

Kutupa vijiwe katika vikuta (viguzo) vitatu navyo ni:-

- Kikuta (kiguzo) kidogo
- Kikuta (kiguzo) cha kati
- Kikuta (kiguzo) kikubwa

Na ufafanuzi kwa kutupa vijiwe katika vikuta (viguzo) hivyo ni kama ifuatavyo:-

1. Atatupa vijiwe katika vikuta hivyo vitatu, kila siku katika masiku ya Tashriq baada ya zawal (kutenguka kwa jua, kwa lugha nyepesi ni kuanza kuingia kwa dhuhri na ipo kauli kua ni saa tano na kuelekea juu) kwa vijiwe saba katika kila kikuta (kiguzo) na atafuata mpangilio wa kuanza na kikuta kidogo kisha kikuta cha kati kisha kikuta kikubwa

2. Ataanza na kikuta (kiguzo) kidogo, anapomaliza kutupa vijiwe atasonga mbele (atasogea) mbele kidogo upande wa kulia, atasimama akielekea kibla kisimamo kirefu akiomba dua, na atanyanyua mikono yake

4. Baada ya hapo atakwenda katika kikuta (kiguzo) cha kati atatupa vijiwe kama alivyotupa katika kikuta kidogo, kisha ataenda upande wa kushoto, asimame kisimamo kirefu huku akielekea qibla na kunyanyua mikono yake akiomba dua.

5. Baada ya hapo atakwenda katika kikuta (kiguzo) kikubwa na kutupa vijiwe, Al-qaaba ikiwa upande wake wa kushoto na Mina upande wa kulia, anapomaliza kutupa vijiwe hapa, hatosimama na kuomba, bali ataondoka na hii ndio sunna.

6. Kisha atatupa vijiwe siku ya pili na ya tatu kwa namna Tuliyoitaja.

7. Atatupa vijiwe akitaka katika sehemu ya juu, ya kati au ya chini kama ilivyojengwa.

KUFANYA HARAKA KUONDOKA KATIKA MWEZI (TAREHE) 12 KATIKA MASIKU YA MINA PAMOJA NA KUWA KUBAKIA HADI MWEZI (TAREHE) 13 NI BORA ZAIDI

Sheria imemruhusu kwa hujaji anaetaka kuondoka katika maeneo ya Mina kabla ya mwezi (tarehe) 13 kama Allah (Subhaanahu wata'ala) alivyosema:-

﴿فَمَن تَعَجَّلَ فِي يَوۡمَيۡنِ فَلَآ إِثۡمَ عَلَيۡهِ وَمَن تَأَخَّرَ فَلَآ إِثۡمَ عَلَيۡهِۚ لِمَنِ ٱتَّقَىٰۗ﴾

"Basi (lakini) mwenye kufanya haraka katika siku mbili (akarejea) si dhambi juu yake, na mwenye kukawia si dhambi juu yake, kwa mwenye kumcha Allah"

- Atakaetupa vijiwe katika masiku ya kumi na moja na kumi na mbili, baada ya hapo akataka kufanya haraka kuondoka Mina basi itajuzu (itafaa) kwake kufanya hivyo bila ya matatizo na atatakikana atoke kabla ya kutua kwa jua la siku ya kumi na mbili.

- Na kwa Yule atakaebaki mpaka tarehe kumi na tatu ili atupe vijiwe siku hiyo, basi kufanya hivyo ni bora zaidi kwake kuliko kuondoka, kwani ndivyo alivyofanya Mtume (swallallahu a'layhi wasallam) pamoja na kuwa aliruhusu watu kuondoka katika tarehe kumi na mbili ila yeye alibaki.

- Lau kama atatupa vijiwe, na kuamua kuondoka tarehe kumi na mbili, jua likatua kabla hajaondoka kwa ajili ya msongamano au sababu nyengine yoyote ile bila ya kukusudia, basi ataondoka na hana dhambi, kwa sababu kuchelewa kwake sio kwa khiari yake.

- Ama aliyebaki kwa khiari yake mpaka jua likatua, hapo itamlazimu atimize na siku ya tatu (tarehe kumi na tatu).

TWAWAAFUL-WADAA (TWAWAAFU YA KUAGA)

Twawaaful-wadaa (twawaafu ya kuaga) imekusanya vipengele hivi vifuatavyo:-

1. Kwanza; Hujaji (Al hajj) anapotaka kuondoka mji wa Makka ni wajibu kwake kutufu twawaaful-wadaa (twawaafu ya kuaga) hata kama ni kwa kubebwa ikiwa hawezi mwendo, liwe jambo la mwisho kwake ni kutufu twawaafu hiyo kwa dalili ya kauli yake Mtume pale aliposema:-

(لاَ يَنْفِرَنَّ أَحَدٌ حَتَّىٰ يَكُونَ آخِرَ عَهْدِهِ الطَّوَافُ بِالْبَيْتِ) (رَوَاهُ مُسْلِم:١٣٢٧) (وَأَبُوْ دَاوُدَ: ٢٠٠٢) وَغَيْرُهُمَا.

“ Asiondoke yoyote mpaka iwe ahadi yake ya mwisho (miadi yake ya mwisho jambo lake la mwisho) iwe ni kutufu nyumba ya Allah (Subhaanahu wata’ala) Al-qaaba’’.

Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) amesema hayo baada ya kuwaona watu wanaondoka katika kila njia kuelekea na kutokutufu twawaafu hii ndiyo Mtume akayasema maneno hayo ili mtu aondoke basi awe ametekeleza twawaafu hii.

Ama watu wa Makkah hawana twawaaful-wadaa (twawafu ya kuaga).

2. Ama mwanamke aliye katika ada yake ya mwezi (heidhi) huyu kwake sio wajibu kutufu twawaaful-wadaa (twawaafu ya kuaga) kwa ruhusa waliyopewa na Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) kwa kauli ya ibnu Abbas (Radhwiyallahu a'nhu) pale aliposema:-

(أَنَّ النَّبِيَّ ﷺ رَخَّصَ لِلْحَائِضِ أَنْ تَصْدُرَ قَبْلَ أَنْ تَطُوْفَ إِذَا كَانَتْ قَدْ طَافَتْ طَوَافَ الإِفَاضَةِ). (أَخْرَجَهُ البُخَارِيُّ : ١٧٦٠)، (وَمُسْلِم :٣٠٩٧) بِلَفْظٍ آخَرَ، وَأَحْمَدُ بِإِسْنَادٍ صَحِيْحٍ عَلَى شَرْطِ الشَّيْخَيْنِ.

" Hakika Mtume (swallallahu a'layhi wasallam) ameruhusu kwa mwanamke mwenye heidhi (ada yake ya mwezi) kuondoka kabla ya kutufu (twawaafu ya kuaga) itakapokuwa mwanamke huyo ameshatufu Twawaaful-ifaadha"

3. Wala sio sawa kwa wanawake walio katika ada zao kusimama mlangoni mwa msikiti ili kuaga msikiti, bali huu ni uzushi usiokuwa na mashiko.

4. Hujaji (Alhaji) atakapomaliza kutufu atatoka na kutembea kama kawaida, kinyume na wanavyofanya baadhi ya watu ambao hutoka huku wakitembea kinyume nyume huu pia ni uzushi.

5. Baada ya twawaafu hii, Hujaji asibaki Makkah ila kwa dharura, kama kukimiwa swala, kusalia jeneza, au kununua zawadi akiwa njiani, ama kubakia bila ya dharura yoyote itabidi arejee tena twawaful-wadaa (twawaafu ya kuaga).

6. Twawaaful-wadaa (twawaafu ya kuaga) ni katika mambo ya wajibu kwa anaefanya ibada ya hijja, na wala sio wajibu kwa anaekwenda huko Makkah kwa ajili ya U'mra, bali hakuna dalili kwa anaekwenda U'mra atatakikana kufanya twawaaful-wadaa

7. Ikiwa hujaji atataka kufanya twawaafu za sunna kabla ya kutia nia ya kutufu twawaaful-wadaa anaruhusika kufanya hivyo, kwa maana yeye kila anapokuja msikitini (msikiti wa Makka) kutokea hotelini akaanza twawafu na kusali rakaa mbili mbele ya maqamu-ibraahim, anaruhusiwa kufanya hivyo na ni bora zaidi ikiwa ana wasaa wa kufanya hayo kabla ya kuingia wakati wa swala au baada ya kuswali swala ya faradhi akaamua kuyafanya hayo pia sharia inamruhusu kufanya hivyo

Ifahamike kuwa kila hujaji twawaafu zake zikiwa nyingi basi thawabu nazo zinaongezeka lakini twawafu hizo ni twawafu za sunna, na miongoni mwa dalili zinazoonesha ubora wa kutufu twawaafu nyingi za sunna ni hadithi ifuatayo:

وَعَن عَبْدِ اللهِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللهِ ﷺ: (مَنْ طَافَ بِهَذَا الْبَيْتِ أُسْبُوعًا فَأَحْصَاهُ، كَانَ كَعِتْقِ رَقَبَةٍ، لاَ يَضَعُ قَدَمًا وَلاَ يَرْفَعُ أُخْرَى إِلاَّ حَطَّ اللهُ عَنْهُ بِهَا خَطِيئَةً، وَكَتَبَ لَهُ بِهَا حَسَنَةً).

"Na kutoka kwa Abdillah bin Omar (Radhwiyallahu a'nhuma) amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallahu a'layhi wasallam) "Yeyote atakaetufu nyumba hii ya Al-qaaba kwa wiki na akaidhibiti wiki hiyo (na ipo kauli kua akaidhibiti twawafu hiyo) inakuwa (katika malipo yake) kama kuacha mtumwa huru,

haweki mguu wake chini (wakati wa kutufu) na wala hanyanyui mguu mwengine (wakati anatufu) isipokuwa Allah anamfutia makosa yake na anamuandikia mema (kwa kunyanyua miguu yake na kuweka chini wakati anatufu Al-qaaba).

Haya ni malipo makubwa sana ambayo yanapatikana katika kutufu Al-qaaba na kila twawaafu zinapokuwa nyingi ndivyo malipo yake yanayokuwa mengi sana. Kwa hiyo ewe ndugu mwislamu unapofika Makkah na ukawa umemaliza ibada yako ya hijja na unasubiri utufu twawaaful-wadaa na ikiwa unazo siku za kubakia pale Makkah basi fika mapema msikitini na tufu twawaafu za sunna kila unapofika msikitini ili upate fadhila hizi kubwa

Baada ya kufanya hujaji haya tuliyoyaeleza mwanzo wa kitabu mpaka kufikia kufanya twawaaful-wadaa hapo itakuwa yametimia matendo ya Hijja.

NA ALLAH NDIE MJUZI ZAIDI.

ZIARA YA (KUTEMBELEA) YA MSIKITI WA MTUME MADINA PAMOJA NA MASJID-QUBAA (MSIKITI WA QUBAA) NA ADABU ZAKE

Kufanya ziara katika msikiti wa Mtume katika mji wa madina ni katika ibada zinazopendezeshwa kwa Muisilamu, tena pendekezo lililokuwa lina mkazo mkubwa sana, kwa hadithi zilizokuja kutoka kwa Mtume (swallallahu a'layhi wasallam) na pia miongoni mwa hadithi hizo zinazoonesha umuhimu wa kuzuru msikiti wa Mtume ni hizi zifuatazo:

عَن أَبِي سَعِيْدٍ الخُدْرِيِّ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللهِ ﷺ: (لاَ تُشَدُّ الرِّحَالُ إِلاَّ إِلَى ثَلاَثَةِ مَسَاجِدَ: المَسْجِدِ الحَرَامِ، وَمَسْجِدِ الرَّسُولِ ﷺ، وَمَسْجِدِ الأَقْصَى) (رَوَاهُ البُخَارِيُّ: ١١٩٠) وَاللَّفْظُ لَهُ (وَمُسْلِم: ٣٣٧٥).

“Kutoka kwa Abuu Said Alkhudriyy (Radhwiyallahu a’nhu) amesema: Amesema Mtume wa Allah (swallallahu a’layhi wasallam): “Pasifungwe safari isipokuwa kuelekea misikiti mitatu, msikiti wa Makkah, msikiti wa Mtume na msikiti wa mbali (Masjidil Aqswaa) (uliopo Jaruselem palestina)”.

وَعَن أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللهِ ﷺ: (صَلاَةٌ فِي مَسْجِدِي هَذَا خَيرٌ مِنْ أَلْفِ صَلاَةٍ فِيمَـا سِوَاهُ إِلاَّ المَسْجِدِ الحَرَامِ). (رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ١١٩٠)، (وَمُسْلِم : ٣٣٧٥).

“Na kutoka kwa Abuu Huraira (Radhwiyallahu a’nhu) amesema: Amesema Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam) “Swala itakayoswaliwa katika msikiti wangu huu ni bora kuliko swala elfu moja zitakazoswaliwa katika misikiti mengine isipokuwa msikiti wa Makkah”.

Hadithi hizi na nyenginezo zinaonesha umuhimu na ubora wa waisilamu kufika katika misikiti mitukufu na kufanya ibada, nayo misikiti hiyo ni hii ifuatayo:

- Msikiti Mtukufu wa Makkah.
- Msikiti Mtukufu wa Mtume (swallallahu a’layhi wasallam).
- Msikiti Mtukufu wa Aqswa (Palestina).

Nasi tupo kuelezea msikiti wa Mtume uliopo katika mji wa Madina ambao muislamu akiswali swala moja tu basi inakuwa bora swala hiyo na kuwa juu zaidi kuliko swala elfu moja zitakazo swaliwa katika msikiti mwengine, kwa hiyo kwa fadhila hizi muisilamu anapofika katika miji ya Saudia asizembee kufika katika msikiti huo na kujichukulia fadhila zilizoandaliwa kwa kila atakaeingia katika msikiti huo na akaswali swala, sawa ziwe swala za sunna au faradhi.

1. Inapendekezwa kwa anaezuru msikiti huu wa Mtume aswali swala zake zote tano, kwa dalili ya hadithi zilizotangulia na kuonesha ujira mkubwa unaopatikana ndani ya msikiti huu kwa yule atakeswali ndani yake.

2. Kuzuru msikiti huu wa Mtume (swallallahu a'layhi wasallam) kunapendezeshwa kwa wanaume na kwa wanawake, wakati wa kufika msikitini hapo sawa ikiwa kabla ya Hijja au baada ya kumaliza ibada ya Hijja.

3. Kuzuru msikiti wa Mtume hakuna mafungamano yoyote na ibada ya Hijja sio katika masharti ya Hijja wala sio katika nguzo za hijja na wala sio katika mambo ya wajibu katika ibada ya Hijja.

4. Anaposwali (anapofika) msikitini, anaezuru msikiti wa Mtume anapendezeshwa atangulize mguu wa kulia wakati wa kuingia msikitini, na asome dua ile ile kama anapoingia msikiti wowote mwengine, wala msikiti wa Mtume hauna dua Makhsusi (maalumu) tofauti na misikiti mengine.

5. Akiingia ndani ataswali rakaa mbili kama anavyofanya akiingia msikiti wowote ule mwengine.

6. Akipata nafasi ya kuswali rakaa mbili katika Raudha tukufu ni bora zaidi kwa dalili ya Mtume (Swallallahu a'laihi wasallam) pale aliposema:

(مَـا بَيْنَ بَيْتِي وَمِنْبَرِي رَوْضَةٌ مِنْ رِيَاضِ الجَـنَّةِ وَمِنْبَرِي عَلَى حَوْضِي).

(رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ٦٥٨٨, ١١٩٦)، (وَمُسْلِم : ١٣٩١) مِنْ حَدِيْثِ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُ.

“Baina ya nyumba yangu na membari yangu ni kiwanja miongoni mwa viwanja vya peponi na membari yangu iko juu ya hodhi langu”

Nimesema hapa (Abuu Muhammad Hasnuu) “Maneno haya ya Mtume wetu yanaonesha kuwa hii ni sehemu tukufu kwa hiyo muislamu ukipata nafasi ya kusali rakaa mbili za faradhi na za sunna katika eneo hilo ni vyema ukafanya hivyo, lakini bila kuwaudhi ndugu zako katika waislamu kwa kupigana vikumbo na kutiana majeraha ama kufanya hivyo ni makosa, na ikiwa wewe huwezi kuswali katika eneo hilo la Raudhwat mpaka uwadhuru waislamu wenzako basi ni vyema kuswali sehemu nyengine ili waislamu wasidhurike na vitendo vya kusukumana na kupiga vikumbo, na hili wengi wa waislamu hawalizingatii, matokeo yake ni kuwaumiza ndugu zao waisilamu au kwa lugha nyepesi ni kuumizana, na ibada kutofanyika kwa utulivu na unyenyekevu ambao unatakikana upatikane ndani ya ibada ya swala.

7. Baada ya hapo anaweza kwenda kuzuru kaburi la Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) na masahaba wake wawili, Abuu bakar na Omar (Radhwiyallahu a'nhuma).

8. Atasimama mbele ya kaburi ya Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) kwa adabu na kushusha sauti yake, kisha atamsalimia kwa kusema:

(السَّلاَمُ عَلَيْكَ يـــا رَسُوْلَ اللهِ وَرَحْمَةُ اللهِ وَبَرَكَاتُهُ).

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

"Assalaamu a'layka yaa rasulallahi warahmatullahi wabarakaatuh"

8. Baada ya kumsalimia Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) atamsalimia Abuu Bakar na Omar (Radhi za Allah ziwe juu yao) kuwaombea na kuwatakia radhi kama alivyokuwa akifanya Abdullahi bin Omar

(السَّلاَمُ عَلَيْكَ يـــا رَسُوْلَ اللهِ، السَّلاَمُ عَلَيْكَ يـــا أَبَابَكْرٍ، السَّلاَمُ عَلَيْكَ يـــا عُمَرُ).

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

"Assalaamu a'layka yaa rasulallahi, Assalaamu a'layka yaa Abaabakar, Assalaamu a'layka yaa Omar"

Baada ya kusalimia ataondoka.

10. Anapotaka kujiombea nafsi yake ataelekea kibla wala sio kaburi, katika sehemu ya kando aombe dua anayotaka kwa maana maeneo ya kaburi awe ameondoka na aelekee kibla na siyo kulielekea kaburi, wakati mtu anapotaka kujiombea dua yeye binafsi na hata kuwaombe wengine.

11. Na inapendezeshwa kwa yule aliyefika mji wa Madina na kufanya ziara, kuzuru na kutembelea msikiti wa Qubaa (Masjid Qubaa) kwa dalili ya hadithi iliokuja inayosema hivi ifuatavyo:

وَعَن عَبْدِ اللهِ بْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا قَالَ: (كَانَ رَسُولُ اللهِ ﷺ: يَأْتِي مَسْجِدَ قُبَاءٍ رَاكِبًا وَمَاشِيًا فَيُصَلِّي فِيهِ رَكْعَتَيْنِ). (رَوَاهُ البُخَارِيُّ : ١١٩٤) (وَمُسْلِم : ١٣٩٩).

“ Na kutoka kwa Abdillahi bin Omar (Radhwiyallahu a’nhuma) amesema: Alikua Mtume wa Allah (Swallallahu a’layhi wasallam) akiujia Masjid-Qubaa (msikiti wa Qubaa) hali ya kuwa yupo juu ya kipando na akiujia hali ya kuwa akitembea kwa miguu (na anapofika msikitini hapo) basi huswali rakaa mbili ndani”

12. Na mtu atakaeswali ndani ya msikiti huo wa Qubaa, malipo ambayo anayapata ni sawa na mtu aliyefanya ‘Umra. Dalili ya hayo ni kauli yake Mtume (Swallallahu ‘alayhi wasallam) pale aliposema:

(مَنْ تَطَهَّرَ فِي بَيْتِهِ ثُمَّ أَتَى مَسْجِدَ قُبَاءٍ فَصَلَّى فِيهِ صَلاَةً، كَانَ لَهُ كَأَجْرِ عُمْرَةٍ). (أَخْرَجَهُ ابْنُ مَاجَةَ ١٤١٢) وَصَحَّحَهُ الأَلْبَانِيُّ فِي صَحِيحِ ابْنِ مَاجَةَ مِنْ حَدِيثِ عَبْدِ اللهِ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا.

“Yeyote atakaejitoharisha nyumbani kwake, kisha akaenda masjid Qubaa akaswali ndani ya msikiti huo swala itakuwa kwake kama malipo ya U’mrah”.

NA ALLAH NDIE MJUZI ZAIDI.

SWALA YA MAITI KATIKA MISIKITI MITAKATIFU MSIKITI WA MAKKAH NA MSIKITI WA MADINAH

Swala ya kuswalia maiti ni swala ambayo watu wengi hawaswali kwa sababu husema hawajui inavyoswaliwa, na wengine huona haina umuhimu wowote na huku huwa wanasema “Kwakuwa baadhi huswali na sisi wengine hatuna haja ya kuswalia” na mfano wa maneno hayo.
Sisi hapa tunapenda kufahamisha umuhimu wa swala hiyo ili mtu atilie umuhimu mkubwa na asiwe ni miongoni mwa wale wenye kupitwa. Na tunaanza kama ifuatavyo:-

- Swala ya maiti ni faradhi kifaya, kwa maana baadhiwakiiswali basi wale waliokuwa hawajaswali dhimma imekwisha ondoka.

- Swala ya maiti hutangulizwa kuswaliwa kuliko swala ya sunna, hili wengi wa watu hawalifahamu huwacha kuswalia maiti wakajishughulisha na swala za sunna.

- Swala ya maiti endapo muisilamu ataiswali basi ujira (malipo) ni sawa na mlima wa Uhudi kwa wale waliofika Madina na wakafika maeneo uliokuwepo huo mlima wanajua ukubwa wa mlima huo, kwa hiyo malipo yake ni makubwa sana.

- Swala hiyo muisilamu ajitahidi kuiswali ili apate yale malipo yalioainishwa na kutajwa na Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam).

Hapa tunaielezea swala ya maiti katika kitabu chetu hichi, kwanza ifahamike swala ya maiti haina mafungamano na ibada ya Hijja, wasije fahamu vibaya baadhi ya waisilamu kuwa miongoni mwa mafunzo ya Hijja ni lazima ujifunze swala ya maiti kwa sababu swala ya maiti imefungamana na ibada ya Hijja. Hapana! ufahamu huu si sahihi na endapo muisilamu atafahamu hivi basi atakuwa amefahamu kimakosa, bali usahihi ni kuwa tunaeleza swala ya maiti kwa sababu, swala hiyo inaswaliwa kwa wingi katika misikiti hiyo kwa hiyo ni vyema kuijua ili akipewa taufiq na Allah ya kufika ndani ya misikiti hiyo hususani kipindi cha Hijja awe na uwezo mzuri wa kielimu katika kuitekeleza swala hiyo. Na hapa naanza kuelezea swala ya maiti kama ifuatavyo:-

NAMNA YA KUSWALI SWALA YA MAITI

Swala ya maiti huswaliwa kwa Takbira nne (4) na ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:-
Baada ya kutoa au kutamka **takbira ya kwanza** utasoma Suratul Fatiha (Alhamdu) mwanzo hadi mwisho wa sura hiyo na pia unaruhusiwa kusoma sura nyengine.

TANBIHI: Kuhusu dua ya kufungulia swala katika swala ya maiti haijathibiti na ndo maana tumesema mtu akitoa takbira ya mwanzo tu atasoma suratul-Fatiha. Kwa hiyo ifahamike kuwa katika swala ya maiti hakuna dua ya kufungulia swala hiyo.

Takbira ya pili: Baada ya kuisoma takbira hiyo utamswalia Mtume (Swallallahu a'layhi wasallam) kama ifuatavyo:-

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّد، كَمَا صَلَّيْتَ عَلَى إِبْرَاهِيْمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيْمَ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ،كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيْمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيْمَ، فِي العَالَمِينَ إِنَّكَ حَمِيْدٌ مَجِيْدٌ.

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

"Allahumma swalli a'laa Muhammad wa'alaa aali Muhammad, kamaa swallayta a'laa Ibraahim wa'alaa aali Ibraahim, wabaarik a'laa Muhammad wa'alaa aali Muhammad, kamaa baarakta a'laa Ibraahim wa'alaa aali Ibraahim, fil-a'alamiyna innaka hamiydum majiydu.

Takbira ya tatu: Baada ya kumswalia Mtume (Swala na salamu ziwe juu yake) utatoa na kutamka takbira ya tatu na baada ya kutamka takbira ya tatu utamuombea dua maiti nayo ni kama ifuatavyo:-

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِحَيِّنَا، وَمَيِّتِنَا، وَشَاهِدِنَا، وَغَائِبِنَا، وَصَغِيرِنَا، وَكَبِيرِنَا، وَذَكَرِنَا، وَأُنْثَانَا. اللَّهُمَّ مَنْ أَحْيَيْتَهُ مِنَّا فَأَحْيِهِ عَلَى الإِسْلاَمِ، وَمَنْ تَوَفَّيْتَهُ مِنَّا فَتَوَفَّهُ عَلَى الإِيْمَانِ. اللَّهُمَّ لاَ تَحْرِمْنَا أَجْرَهُ وَلاَ تُضِلَّنَا بَعْدَهُ.

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

"Allahumma ighfir lihayyinaa, wamayyitinaa, washaahidinaa, waghaaibinaa, waswaaghiirinaa, wakabiirina, wadhakarinaa, wa unthaanaa. Allahumma man ahyaytahu minnaa faah-yihii a'lal-

islaam, waman tawaffaytahuu minnaa, fatawaffahuu a'lal-iimaan, Allahumma laa tahrimnaa ajrahuu, wala tudhwillanaa ba'adahu"

Takbira ya nne: Pia utamuombea maiti dua, kwa hiyo utairejea hiyo hiyo katika takbira ya nne au dua nyengine katika zile zilizothibiti kumuombea maiti.

FAIDA:

Dua za kumuombea maiti zimekuja nyingi sana kutoka kwa Bwana Mtume (swallallaahu a'layhi wasallam) kwa maana zimethibiti ila sisi tumeichagua dua hii ambayo tumeielezea na kuitaja hapo juu ni kwa sababu duo hiyo imekusanya sifa zote za maiti, nakusudia maiti akiwa mmoja au wengi, au akiwa mwanamme au mwanamke, basi dua hii inajitosheleza wala huhitaji kubadilisha dhamiri ya umoja kwenda wingi bali uombe dua hii kama ilivyo.

Na pia tumeichagua dua hii kwa sababu katika msikiti wa Makkah na Madina maiti huwa ni wengi katika kipindi cha Hijja kwa hiyo hii ni dua muafaka.

TANBIHI:

a) Neno "Dhamiri" maana yake ni kiwakilishi cha jina.

b) Ikiwa mtu anakwenda kumuhijia mtu mwengine, basi matendo yote yatakuwa ni hayo hayo ila kwenye nia na kutamka Hijja ndo atasema kama ifuatavyo:-

لَبَّيْكَ اللَّهُمَّ حَجًّا عَنْ فُلاَنٍ.

WASIOJUA KIARABU WATASEMA

"Labbayka Allahumma hajjan a'n fulan"

Kwenye tamko **“AN FULAN”** atamtaja huyo anaemuhijia kwa maana atalitaja jina la anaehijiwa, kisha matendo yote atayafanya kama tulivyoeleza mwanzo hadi mwisho wake.

Mwisho kabisa tunamuomba Allah mtukufu kwa majina yake matukufu na sifa zake nzuri awanufaishe waisilamu kupitia kitabu hichi, na akifanye kuwa ni nuru kwa mas-ala haya ya Hijja, na ajaalie haya tuliyoyaandika yawe katika mema yetu siku ya kukutana nae (Allah), na atukutanishe na Bwana Mtume (Swallallahu a’layhi wasallam) pamoja na maswahaba zake katika pepo ya Firdaus.

(Aamin).

KIMEANDIKWA NA KUTAYARISHWA NA

ABUU MUHAMMAD HASNUU AMOUR KOMBO

AZZINJIBARY ATTANZANIY

MAKTABATUL IMAMIL AUZAAI'Y
ZANZIBAR TANZANIA
0779819880 0772719464
0776959197